**MWINYI** asisitiza uimara mifumo utoaji wa haki



UKURASA 2

**MFANYABIASHARA** ajiua kwa kujipiga risasi kichwani



UKURASA 4

**CHENJI** 2,500/- baa yakatisha uhai wa mtu

UKURASA 4



**BARCA** yafikiria kumuuza Pedri

UKURASA 22

Nipashe

Jumamosi Machi 9, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581610

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# CHADEMA yaibua upya hoja kikokotoo mafao

UKURASA 2



Askari polisi wa kike wa wilaya ya Urambo mkoani Tabora, wakionyesha uwezo wao wa kuruka kabla ya kuanza kufanya usafi katika eneo la makao makuu ya wilaya hiyo, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikakati yawekwa kuinua wanawake

**UDSM** kuwapandisha chati, TANAPA yaona fursa...

*Endelea ukurasa wa 3 & 5*



## ACT-Wazalendo yatishia kujitoa Serikali ya Umoja Kitaifa Zanzibar

UKURASA 2

**MICHEZO** **MGUNDA AKANUSHA KUTAKIWA SINGIDA** UK. 23

**KATUNI** UK. 6



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mobility Group, Ahmed Abood, akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha Rais mstaafu, Hayati Ali Hassan Mwinyi katika ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchi za Falme za Kiarabu, Abu Dhabi, alipofika kutoa pole jana. **PICHA: UBALOZI**

# CHADEMA yaibua kikokotoo mafao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema Bunge lililopitisha Sheria ya Wenza wa Viongozi kulipwa mafao, linapaswa kufanya marejeo ya Sheria ya Kikototoo cha Mafao ambacho kinalalamikiwa na watumishi.

Vilevile, kimesema katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika mwaka huu na mwakani, utakuwa wa kufa na kupona kwa kuwa kitaweka wagombea kila nafasi itakayotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), Catherine Ruge, alisema hayo jana jijini hapa kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyoandaliwa na chama hicho.

"Wananchi wengi bado wanakabiliwa na shida nyingi sana ikiwamo afya, huduma za maji, miundombinu na kupanda kwa gharama za maisha, lakini leo Bunge linapitisha sheria ya wenza wa viongozi kulipwa mafao.

"Wako watumishi wa umma kwa mfano, muuguzi wa ngazi ya cheti analipwa mafao ambayo hayaeleweki, lakini leo hii Bunge linapitisha sheria ya wenza wa viongozi kulipwa mafao," alisema Ruge.

Alisema BAWACHA inashauri Bunge kufanya marejeo ya sheria ya kikokotoo ambayo yatawezesha kufanyika kwa maboresho ambayo yataleta ahueni kwa Watanzania wa hali ya chini.

"Bunge lipo kwa ajili ya kutetea wananchi wanyonge siyo watu watatu ambao ni wenza wa viongozi wanaotaka leo waume zao walipwe na wao walipwe pia," alisema.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alisema uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, utakuwa wa kufa na kupona, hivyo hakuna mgombe yeyote wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) atakayekosa mpinzani kutoka chama hicho kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita.

Mbowe alisema katika uchaguzi huo, CHADEMA imepanga kuweka mgombea kila nafasi itakayotangazwa na NEC katika ngazi zote kuanzia kitongoji hadi taifa.

"Uchaguzi ujao utakuwa wa kufa na kupona. CHADEMA tutahakikisha tunaweka wagombea kila nafasi itakayotangazwa. Lazima kila mgombea atakayejitokeza CHADEMA tuwepo pale kumpinga, hakuna kupita bila kupingwa," alisisitiza Mbowe.

Mwenyekiti huyo alimwagiza Katibu Mkuu, John Mnyika, kuhakikisha mfumo mzima wa chama kila eneo anapatikana kiongozi bora na sio bora kiongozi. "Lazima mhakikishe kila eneo anapatikana mtu wa kwenda kugombea na awe na uwezo wa kushinda siyo kushiriki na kwa kiongozi yoyote ambaye atashindwa kuweka mgombea.

"Chama hatutamchekea katika hilo, tutachekea kwa mambo mengine siyo hilo, lazima tuwe na uchungu. Sisi ndiyo tutaweza kuondoa huu msiba wa CCM," alisema.

Mbowe alisema CHADEMA ndicho chama pekee ambacho kitakwenda kumaliza malalamiko ya wananchi ambayo hivi sasa wanalalamikia ugumu wa maisha. Alisema wanachoomba ni Tume Huru ya Uchaguzi na Katiba Mpya kwa kuwa ndiyo itasaidia kumaliza tabia ya kuingia madarakani kwa viongozi ambao hawana kibali cha watu na Mungu.

"Asilimia 90 ya viongozi walioko madarakani hivi sasa wengi wao wameingia katika nafasi hizo kwa njia zisizo za haki kutokana na uwapo wa tume hii ya uchaguzi, hali ambayo imesababisha uwapo wa ufisadi, uminyaji haki na uvunjifu wa demokrasia nchini," alisema.

Alisema hivi sasa wananchi wanalalamikia gharama za maisha kupanda, lakini wabunge ambao wamechaguliwa kuwawakilisha wanajiongezea mishahara.

"Mfumuko wa bei umepanda mara tatu, lakini wabunge mwaka jana wamejipandishia mishahara hadi milioni 18 kwa mwezi," alisema Mbowe.

Awali, Mwenyekiti wa BAWACHA, Sharifa Sulaiman, alisema wanawake wengi wameonyesha nia ya kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu ujao ikiwamo nafasi ya urais.

Alisema wanachosubiria ni ridhaa ya chama na wataendelea kuwahamasisha ili wengi kujitokeza katika nafasi mbalimbali.

# Mwinyi asisitiza uimara mifumo utoaji wa haki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mifumo ya utoaji haki inapaswa kuimarishwa kwa kuzingatia urahisi wa wananchi hasa wenye mahitaji maalum katika kuzifikia huduma za kisheria.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akifunga mkutano wa mawaziri wa sheria wa nchi wanachama wa Jumuiya za Madola.

Mwinyi alizitaka nchi wanachama kuzingatia matumizi ya mifumo ya kidigitali ili kuimarisha utawala wa sheria na upatikanaji wa haki.

Alisema serikali zote mbili ya Zanzibar na Tanzania zimechukua hatua katika kuhakikisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria unatamalaki.

Alitaja hatua hizo ni kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria lakini pia kuanzisha programu zinazorahisisha utekelezaji wa utawala wa sheria kama vile programu ya msaada wa sheria na marekebisho ya sheria za kodi na uwekezaji katika pande zote.

"Kufanyika mkutano huo Tanzania hasa Zanzibar kunatoa fursa ya wataalamu wetu wa sheria kupata ujuzi na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa haki kwa kuwawezesha kuzifikia na kutoa ushahidi kwa njia ya kidigitali," alisema.

Dk. Mwinyi alisema serikali inatarajia kujenga kumbi kubwa za mikutano ili kutoa fursa kwa taasisi za kimataifa kufanyia mikutano kutokana na maombi mengi yanayowasilishwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema katika siku tano za mkutano huo, wajumbe wamajadiliana kuhusu namna ya kusaidiana kuzikabili changamoto zinazowakabili nchi wanachama katika matumizi ya teknolojia katika kurahisisha upatikanaji wa haki.

Suleiman alisema hatua zilizofikiwa katika kuimarisha sekta ya sheria na mifumo ya upatikanaji wa haki Zanzibar ni pamoja na kuongezeka kwa bajeti ya mfumo wa mahakama hadi kufikia asilimia sita na ongezeko la majaji wa mahakama kuu waliofikia 14 wakiwamo wanne wanawake.

Hatua nyingine alisema ni mpango wa ujenzi wa mahakama katika kila wilaya uliolenga kupunguza masafa na kupunguza mrundikano wa kesi katika mahakama za mikoa na mahakama kuu, jambo linalochelewesha haki kupatikana kwa wakati.

# ACT yatishia kuvunja 'ndoa' Umoja wa Kitaifa Zanzibar

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetishia kujitoa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar kwa madai kuwa serikali hajjayafanyia kazi mambo waliyokubaliana awali.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, Ado Shaibu, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Shaibu alisema Halmashauri Kuu ya Taifa ya ACT-Wazalendo, ilifanya tafakuri ya kina kuhusu mwenendo wa serikali ya umoja wa kitaifa Zanzibar na kubaini kwa miaka minne hakuna kilichofanyika.

Alisema chama hicho kiliingia katika serikali hiyo kwa kuwa yalikuwa matakwa ya sheria na kwa kuzingatia makubaliano baina ya aliyekuwa mwenyekiti wake, Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye kwa niaba ya chama, aliwasilisha kwa Rais wa Zanzibar hoja tatu ambazo naye alikubali kuzifanyia kazi.

Shaibu alikumbusha hoja hizo kuwa ni kuachiwa huru kwa wafuasi wote wa chama hicho waliokuwa wanashikiliwa na vyombo vya dola kwa sababu za kisiasa.

Nyingine ni kuundwa kwa tume yenye hadhi ya kijaji kuchunguza mauaji yote na ukiukwaji wa haki za binadamu na hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika. Alisema hoja ya tatu ni mageuzi ya mfumo wa uchaguzi katika upande wa Zanzibar akisisitiza kuwa ni jambo ambalo Rais Hussein Ali Mwinyi aliahidi kulitekeleza.

"Sasa muda umepita, miaka minne imepita, tathmini yetu ya ndani, hoja hizi zote tatu ukiachana kipengele cha kuachiwa huru viongozi na wanachama wetu waliokuwa wanashikiliwa na vyombo vya dola.

"Yale mambo ya msingi yanayohusu mageuzi ya kimfumo ya uchaguzi na fidia za waathirika hayajatekelezwa hata moja," alisema.

Shaibu alisema kupitia hatua hiyo wameielekeza Kamati ya Uongozi Kitaifa kukutana na Rais wa Bara na Zanzibar kuwaeleza kuhusu uamuzi wa chama kujitoa katika serikali ya umoja wa kitaifa huku akisisitiza kuwa jambo hilo litafanyika mapema.

"Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 tulizika wafuasi wa chama chetu 24, hii ni idadi kubwa sana ya watu kupoteza maisha katika chama cha siasa nchini. Wapo wenye ulemavu wa kudumu, wapo wanaoishi na risasi mwilini mpaka leo," alisema Shaibu.

Kiongozi huyo pia, alisema Halmashauri Kuu ya Chama imefanya uchaguzi wa wajumbe wa Kamati Kuu ya chama wa kuchaguliwa kutoka kwenye kanda 10.

Alisema kwa kuzingatia madaraka yake chini ya Ibara ya 87(1), na 76(1)(b) ya Katiba ya ACT Wazalendo, Halmashauri Kuu ya Chama Taifa imeidhinisha uteuzi wake kuwa Katibu Mkuu wa chama kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Imemteua Wakili Bonifas Mapunda kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa chama na Aidan Mapunda, katika nafasi ya Idara ya Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma.

# TANAPA yaona fursa Siku ya Wanawake

**Na Maulid Mmbaga**

SIKU ya Wanawake ambayo huadhimishwa Machi 8, kila mwaka, imesherehekewa kwa staili tofauti huku Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ikigeuza kuwa fursa kwa wanawake kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

TANAPA ambayo inasimamia shughuli za uhifadhi na utalii ambazo zinachangia asilimia 17.5 za pato la taifa, ni miongoni mwa mashirika yaliyoona fursa katika siku hiyo baada ya kuitumia kwa kupeleka wanawake kutalii katika hifadhi hiyo ambayo ni ya kwanza kwa ukubwa nchini.

Kwa mujibu wa TANAPA, wanawake wanaopata fursa ya kwenda kwenye hifadhi hiyo, wataona wanyama na vivutio mbalimbali vilivyomo kwa lengo la kutangaza uhifadhi na kuvutia wawekezaji kuchangamkia fursa zinazopatikana katika sekta hiyo.

Kamanda wa Uhifandi Kanda ya Kusini, Steria Ndaga, alisema wanawake ni wengi, hivyo kwa umoja wao wakiitumia fursa hiyo vizuri, wataendeleza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amehakikisha kwamba uhifadhi wa mazingira unaendelezwa nchini.

"Lengo ni kuhamasisha wanawake ili kushiriki katika utalii na uhifadhi na umuhimu wake. Tunatembelea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ili kuona vivutio mbalimbali vilivyoko na kutoa taarifa za vivutio vya taifa. TANAPA tunashirikiana na wenzetu wa Chama cha Wanawake wa TAZARA (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia).

"Tukiunga mkono kwa pamoja shughuli hizi za uhifadhi tutaongeza uchumi wetu na taifa kwa ujumla," alisema Ndaga.

Alisema wanahamasisha wanawake wengi zaidi kujitoa na kuona umuhimu wa kushiriki katika uhifadhi nchini kwa kutembelea hifadhi hiyo kwa kuwa iko karibu na miji mikubwa kama Der es Salaam, Pwani, Morogoro, Ruvuma, Lindi na Mtwara na ni rahisi kufikika.

Alisema gharama ya mtoko huo kwa mtu mmoja ni Sh. 200,000 ambayo itahusisha huduma zote zikiwamo utalii wa siku nzima, usafiri na chakula.

Judith Ligenzi, ambaye ni dereva wa treni za TAZARA, aliwahamasisha wanawake kujitokeza kwa wingi kuona kazi za wanawake wenzao kwa kuwa wengine wanasikia kuna madereva wanawake wanaendesha treni na wengine hawaamini.

"Niwahakikishie tupo na tunajiamini na tutaendesha treni kutoka Dar es Salaam hadi Nyerere na kurudi tukiwa salama na tumeona tutengeneze hii kwa sababu reli yetu ya TAZARA inapita mbugani na watu watatumia usafiri wa treni ni kilometa 200 kufika eneo la hifadhi," alisema.

Ligenzi alisema katika safari hiyo, kutakuwa na wanawake kutoka makundi mbalimbali kama taasisi, mashirika na vyuo, huku akisisitiza wengi kujitokeza kutumia fursa hizo kila zinapojitokeza ikiwamo kutumia usafiri wa treni na kutembelea hifadhi.

Zuhura Bakari, mmoja wa wanawake wanaounga mkono jitihada za uhifadhi na utalii, alitoa ujumbe kwa wanawake wenzake akiwasisitiza kutumia siku hiyo katika kutangaza utalii wa ndani hasa kwa wanafamilia angalau kutenga siku moja kwa ajili ya kutembelea vivutio vya utalii.

"Sisi wanawake ndio tunalea familia sasa ni wajibu wetu pia tunapohitaji kupumzika na familia zetu, basi tutenge angalau siku moja ya kutembelea vivutio vya utalii hii itasaidia zaidi kutangaza utalii wa ndani," alisema Zuhura.




Baadhi ya wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, wakiwa wenye furaha, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, katika ofisi za TGL, Mikocheni Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# UDSM yaanika mikakati kuwainua wanawake

**Na Romana Mallya**

UCHACHE wa wanafunzi wa kike katika mitaala ya sayansi na ugumu wa wanawake kuandaa maandiko ili kupanda vyeo kitaaluma, ikiwamo ngazi ya uprofesa, umekifanya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kuweka mikakati maalum ili kundi hilo kuwa kinara.

Katika mahojiano na mwandishi wa habari hizi juzi kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, Naibu Makamu Mkuu wa UDSM (Taaluma), Prof. Bonaventure Rutinwa, alisema chuo kina dira na mpango mkakati unaohimiza usawa wa kijinsia katika elimu na haki sawa za kupata elimu.

"Hilo ndilo tunaloliunga mkono kama sehemu ya sera na mikakati kadhaa inayotusaidia katika kutekeleza hiyo sera.

"Kuhusiana na takwimu zilivyo, kwa sasa chuo kimepiga hatua kubwa sana. Tuna wanafunzi wanaozidi 35,000 na kati ya asilimia 48 ni wa jinsia ya kike. (Takwimu hizi) zingekuwa kubwa zaidi ila zinashushwa na uchache wa wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi.

"Kwa mfano, ukiweka mitaala ya sayansi kando, asilimia ingeweza kufika 60 na zaidi. Tunafanya jitihada makhsusi ya kuhakikisha wanafunzi wanaokuja kusoma sayansi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaongezeka.

"Kwa mfano, tumeweka scholarship (udhamini) ambayo Merit Scholarships (wanafunzi wenye ufaulu mzuri) tumezitenga za wanawake mahususi. Katika scholarships 60 tunazozitoa kila mwaka, nusu lazima wawe wanawake," alisema.

Prof. Rutinwa alisema wameanza mpango wa kuzunguka shule za Tanzania huku wakitumia wataalamu wanawake waliosoma masomo hayo kuhamasisha wanafunzi kusoma sayansi ili kuondoa dhana kuwa suala hilo ni wanaume peke yao.

Alisema kwa mwaka jana wamewafikia wanafunzi 8,000 katika mikoa mitano ambako walihamasisha kuwa sayansi inawezekana.

"Tukifanikiwa katika hili, ule usawa tunaolenga wa asilimia 50/50 angalau katika masomo ya sayansi tutaupata," alisema Prof. Rutinwa.

**UONGOZI**

Kuhusu nafasi ya uongozi chuoni hapo, alisema wamepiga hatua kwa kufikia asilimia 50 kwa 50, kwa maana ya wakuu wa vyuo vishiriki, wakuu wa ndaki, shule kuu asilimia 50 ni wanawake.

"Kwa upande wa uongozi tumefanya vizuri, kwa upande wa taaluma hizo ndizo changamoto. Wito wetu kwa wanawake katika muhktadha wa elimu.

"Wanawake watumie fursa zote zilizoko za kielimu ikiwamo katika masomo ya sayansi na hisabati kwa sababu inawezekana na wana uwezo sawa na wenzao wa kiume hivyo watoe mchango wao katika ujenzi wa taifa," alisema.

**KIKWAZO UPANDAJI VYEO**

Prof. Rutinwa alisema: "Kwa mfano, kikwazo kikubwa katika kupanda vyeo chuoni hapa ni cheo chako cha kitaaluma, huwezi ukawa Mkuu wa Kitivo au Makamu Mkuu wa Chuo kama haujawa Profesa.

"Uprofesa hautegemei uwezo wako wa uongozi. Unategemea uwezo wako wa kitaaluma uandike machapisho. Sisi wanaume ni rahisi kufanya hivyo kwa kuwa tuna muda huo. Wanawake wakitoka hapa (chuoni) wana shughuli nyumbani zinazowabana.

"Katika kuwasaidia, kwa miaka mitatu mfululizo tumeandaa mpango maalum wa kambi ya uandishi ya wanawake, kila mwaka tunawatengea muda, tunawapa fedha wanajifungia mahali wanaandika maandiko. Sasa wanapanda vyeo kwa kipindi hiki tofauti na nyuma."

**RUSHWA YA NGONO**

Prof. Rutinwa alisema chuoni hapo kuna sera kuhusiana na masuala haya ya rushwa ya ngono ambayo inapiga marufuku na kutoa adhabu kali yanapojitokeza.

"Tunawahimiza na kuwawezesha wale wa jinsia ya kike kwamba, unaweza kufanya vizuri na ukawa yeyote bila kutumia masuala ya ngono.

**MWANAMKE KIONGOZI**

Aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, ambaye ni mwanzilishi wa Programu ya Mwanamke Kiongozi, alisema baada ya kuanzisha baadhi ya wanawake walihamasika wenyewe na wengine walijitokeza kwa kuhamasishwa.

"Kwanza inatakiwa kuwapo kwa elimu kutambua nafasi ya mwanamke. Kutambua mwanamke ana uwezo, kuwatia moyo kwamba wanaweza, lakini watakutana na changamoto ila watambue changamoto ni sehemu ya uongozi.

"Ndio maana nilishawishika kuanzisha programu hii ya Mwanamke Kiongozi, na tulitoa mafunzo kwa wanawake zaidi ya 300 kwa kuamini wanaweza na ni sawa na wanaume.

"Kinachotakiwa ni kuwapa nafasi ili kuonyesha uwezo wao. Niseme wanawake ni watendaji wazuri, waaminifu, wachapakazi, wana bidii ya kazi na wanaweza kufanya zaidi ya shughuli moja kwa wakati mmoja. Wanaume wao ni shughuli moja baada ya nyingine," alisema.

Dk. Mlimuka ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Tume ya Ushindani (FCC), alisema ni suala la wanaume kuamini kuwa wanawake wanauwezo sawa na wao vivyo hivyo kwa wanawake na wasikubali kudogoshwa.

"Kwa wanaoamini rushwa ya ngono ili kufanikiwa kushika nafasi, hilo ninalipinga ni rushwa mbaya kabla sijakwenda ATE nilikuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwenye uongozi wangu tulipambania hili. Mwisho wa siku unakuta wanapewa nafasi wasiostahili," alisema.

# Mfanyabiashara adaiwa kujiua kwa risasi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MFANYABIASHARA maarufu Urambo mkoani Tabora, Ramadhani Ntunzwe (53), anadaiwa kujiua kwa kujipiga risasi kichwani akiwa nyumbani kwake.

Kutokana na kifo hicho, Jeshi la Polisi limesema linaendelea kuchunguza chanzo chake.

Wakisimulia tukio hilo, mashuhuda na ndugu wa mfanyabiashara huyo, akiwamo binamu wake, Nyangoma Lubungira, walisema huenda uamuzi huo umefanyika kutokana na kifo cha kaka yake kilichotokea juzi mkoani Kigoma.

"Hatujajua sababu lakini baada ya kupokea taarifa ya msiba wa binamu yake huko Kigoma, aliagiza maduka yake yafungwe ili kujiandaa na safari. Baada ya muda tukashangaa kupata taarifa za kifo chake pia," alisema Lubungira.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Urambo Kati, Sudi Sadiki, alikiri kuwa na taarifa ya kifo hicho alizozipokea kutoka kwa ndugu wa marehemu na majirani baada ya kumpigia simu. Sadiki alisema baada ya taarifa za kifo hicho, alipofika eneo la tukio na kushuhudia ndipo alipotaarifu Jeshi la Polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Richard Abwao, alisema tukio hilo lilitokea Machi 6, mwaka huu, saa 2:00 asubuhi katika Mtaa wa Urambo Kati, Tarafa ya Urambo wilayani humo.

Alisema mfanyabiashara huyo alijipiga risasi moja kichwani akitumia silaha aina ya bastola Pietro Beretta Chinesse yenye namba za usajili h57086ycat5802.

Kamanda Abwao alisema silaha hiyo alipatiwa na mamlaka husika kwa taratibu halali na kwamba jeshi hilo linaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha tukio hilo. Abwao aliwataka wamiliki wa silaha kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ambayo ni kujilinda na si kujitoa uhai kinyume cha lengo kusudiwa.

"Silaha kazi yake ni kujilinda na si kumdhuru mtu wa aina yoyote au kumuua, kujitoa uhai. Hilo ni kosa kisheria na hata kujaribu kujiua," alikumbusha.

Majirani wa mfanyabiashara huyo, walieleza kusikitishwa na kifo cha mfanyabiashara huyo wakimtaja kuwa na bei za tofauti zilizo na pungufu katika maduka yake na kuwa mkombozi kwa wajasiriamali.

Walisema maduka yake yalikuwa na bei za chini tofauti na mengine na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kujipatia faida na alikuwa akitoa msaada kwa makundi mbalimbali ya watu wasiojiweza pamoja na kuwafuturisha waumini katika mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, SACP Benjamin Kuzaga (katikati) na Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani ya Mkoa huo, Mhandisi Rajab Ghuriku, wakikata utepe jijini Mbeya juzi, kuzindua pikipiki mbili zilizotolewa na kamati hiyo, kwa jeshi hilo kwa ajili ya operesheni kwenye barabara kuu ili kupunguza ajali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Chenji ya 2,500/- yasababisha kifo

**Na Samson Chacha,** TARIME

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, linamshikilia mkazi wa kijiji cha Forodhani, Kata ya Sirari, Michael Mwita, kwa tuhuma za kumuua kwa kumchoma kisu mtoto wa mwenye baa, Thomas Nchama, baada ya kuzuka ugomvi kati yao wa kudaiana chenji ya Sh. 2,500.

Mwita aliomba kurudishiwa chenji hiyo kutoka kwa mhudumu ndipo ugomvi ulipozuka na kusababisha kifo hicho.

Diwani wa Sirari, Amos Sagara na Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Wakuru Mirumbe, walisema tukio hilo lilitokea juzi usiku katika baa ya baba wa marehemu.

"Uongozi wa Kata yetu Sirari tunatoa wito kwa vijana kuacha kutembea na silaha kama vile kisu na panga, silaha hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa madhara makubwa yakiwamo mauaji katika kata hii.

"Tunawahimiza askari wa akiba mgambo kwa kushirikiana na vikundi vya ulinzi shirikishi na jeshi la polisi na wananchi kutoa taarifa za uhalifu ikiwamo wanaotembea na silaha," walisema.

Viongozi hao walisema hivi karibuni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Gwitanka, Michael Magasi, wakati wakienda kumkata mtuhumiwa, Sinda Bhoke, katika kilabu cha pombe maeneo ya Sokoni Sirari, anayetumiwa kwa wizi wa simu na fedha alichomwa kisu na kupoteza maisha.

"Visa vya watu kuchomwa kisu vimekuwa vingi katika kata hii, tunawaomba na kuwahimiza wenyeviti wa vitongoji na vijiji katika kata hii waitishe mikutano ya hadhara kukemea vitendo hivi vya mauaji," walisema viongozi hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Michael Njera, amethibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kwamba wanamshikilia Mwita kwa uchunguzi zaidi.

Kamanda Njera alitoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi badala yake kufikisha masuala yao katika vyombo husika ili kutatuliwa.

# Majaliwa aagiza msaada waathirika wa mvua Lindi

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza watendaji wa serikali wanaosimamia urejeshaji wa hali katika maeneo yaliyoathiriwa na mvua mkoani Lindi kuharakisha na kupeleka msaada wa chakula kwa waathirika.

Ameiagiza timu ya wataalam ihakikishe maeneo ambayo hayana huduma kutokana na athari hizo yanapatiwa msaada wa haraka wa chakula kwa kutumia usafiri wa magari ya jeshi na helikopta. Maagizo hayo aliyatoa juzi katika kikao kilichofanyika Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu Oysterbay, Dar es Salaam, wakati akipokea taarifa ya athari za mvua mkoani humo. Kikao hicho kiliwahusisha pia mawaziri, makatibu wakuu na wataalamu wengine wa serikali.

Majaliwa alisema kuwa kutokana na kukatika kwa mawasiliano ya barabara na baadhi ya maeneo ya Chibutuka na Nangano kutofikika kabisa, timu hiyo ya wataalamu ihakikishe maeneo hayo yanapatiwa msaada wa haraka wa chakula.

"Malori ya jeshi yatumike kufikisha vyakula vya msaada wa maafa hadi maeneo ya karibu kwa ajili ya kuwezesha ubebaji wa vyakula hivyo hadi maeneo yenye uhitaji kwa kutumia helikopta," ALISEMA.

Alisema kutokana na Wilaya ya Liwale kutofikika kwa barabara zilizokuwa zikitumika awali, wataalamu waweke jitihada za kuifungua barabara ya Nangurukuru - Liwale.

Pia alisema waangalie namna ya kuwezesha barabara ya Ruangwa- Nangurugwai - Mbwemkuru - Miluwi - Kiangara kuwa njia mbadala ili kusaidia kuifungua Wilaya ya Liwale kutokana na barabara hiyo kuathirika kidogo.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema kuwa wanaendelea kusimamia maelekezo ya viongozi wa kitaifa ili kuhakikisha maeneo yote yenye changamoto yanapatiwa ufumbuzi na kuweza kufikika kama ilivyokuwa awali.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema serikali imejipanga kuwasaidia wananchi wote ambao maeneo yao hayapitiki na wanakosa huduma muhimu za kijamii.

"Tumeweka mpango wa kuwasaidia kuhakikisha wanapata chakula kitakachowasaidia hadi pale miundombinu itakapoimarika, tutaanza kutoa magari mengine ya chakula kutoka Dar es Salaam," alisema.

# 30 waugua kipindupindu, wanne walazwa hospitalini

**Na Jaliwason Jasson**, BABATI

WATU 30 wameripotiwa kuugua kipindupindu huku wanne kati yao wakilazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara.

Januari 9, mwaka huu, ugonjwa huu uliripotiwa kuibuka katika Mkoa wa Mwanza na siku tano mbele watu watano waliugua katika Mji Mdogo wa Kagonga, mkoani Shinyanga ambapo watu 13 walilazwa na 452 waliochangamana walikuwa katika ufuatiliaji.

Kwa mujibu wa Ofisa Afya wa Mkoa wa Manyara, Suten Mwabulambo, hadi sasa waliopata matibabu na kuruhusiwa kurejea nyumbani kujiuguza, ni watu 26.

Taarifa rasmi za kuwapo kwa mlipuko huo wa kipindipundi zilitolewa jana katika Mji wa Babati na Mwabulambo, wakati akiwasilisha taarifa yake kwa Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga.

Mwabulambo alisema ugonjwa huo uligunduliwa Januari 26, mwaka huu, katika Mji Mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro.

"Ingawa mlipuko wa ugonjwa huu, umefanya idadi ya watu waliougua kufikia 30, bado hakijatokea kifo chochote kwa mkoa wetu," alisema.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, walipokea mgonjwa mmoja, Halmashauri ya Mji wa Babati wagonjwa 11 na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, walipokea wagonjwa tisa. Ofisa huyo alisema Wilaya ya Simanjiro ndiyo iliyokuwa ya kwanza kupokea mgonjwa wa kipindupindu na kwa sasa wameweza kuudhibiti ugonjwa.

Alisema katika kudhibiti ugonjwa huo, timu za kudhibiti magonjwa ya mlipuko ziliundwa na zimefanya kazi ili usiingie wilaya zingine.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, ameeleza kuwa wataalamu wa afya wanafumbafumba kuhusu mlipuko wa kipindupindu ambao chanzo chake ni kula kinyesi.

Queen alisema kutokana na mlipuko huo, ameagiza kuhakikisha vyoo vinakuwa safi na salama na siyo mpaka viwe vya kuvuta.

# Taasisi yaadhimisha siku ya wanawake na wachuuzi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Women Tapo, imeadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kujumuisha wachuuzi huku ikihimiza Watanzania kutumia fursa za kupata matibabu na kujua hali za afya zao.

Katika maadhimisho hayo yaliyofanyika jana kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Women Tapo, Lulu Nyapili, alisema kambi mbalimbali zinazowekwa kwa ajili ya wananchi zitawawezesha Watanzania kujua afya zao, hivyo kujiongezea ufanisi katika kazi zao.

Alisisitiza kuwa afya ni mtaji, hivyo mtu kupima na kujua afya yake kutamwezesha kupata matibabu kwa haraka na kwa uhakika. Taasisi hiyo ilifanya maadhimisho hayo kwa upimaji bure wa afya kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anatamani kuona wanawake wakiinuka kiuchumi.

Lulu alisema taasisi hiyo imejikita kuelimisha wanawake wanaofanya shughuli zao sokoni, kama vile mama lishe na wafanyabiashara wadogo wadogo, kuhusiana na unyanyasaji wa kijinsia, rushwa ya ngono, kutambua haki za ardhi na jinsi ya kujikwamua kiuchumi.

Katika kufanya hivyo, alisema taasisi imewafikia wanawake wa Jimbo la Ilala na sasa inajipambanua kuwafikia wanawake wa mkoa mzima wa Dar es Salaam na Tanzania nzima.

Mmoja wa wanufaika wa taasisi hiyo, Edna Mkono, alishukuru Women Tapo kwa kumwezesha mtaji na kupata elimu kuhusu ujasiriamali na kwamba alianza kupatiwa mtaji wa Sh. 50,000 na sasa umekua hadi Sh. 150,000.

Mratibu wa Afya ya Jamii, Dk. Asha Mahita, aliwataka wanawake kuangalia afya zao mara kwa mara kwa kuwa mwanamke ni afya.

"Mwanamke thamini afya yako kwani afya yako ndio mtaji wako. Wanawake tuwekeze kwenye afya," alisema.

Pamoja na upimaji wa saratani ya matiti na mlango wa kizazi, wanawake waliofika katika viwanja hivyo walikutana pia na madaktari mbalimbali wa magonjwa ya afya ya akili ambayo imeelezwa kuwa wanne kati ya wanawake 10 wanaonekana kuwa na tatizo hilo.

Meneja wa Kampuni ya Vertex ambayo iliratibu upimaji afya kwa kushirikiana na Hospitali ya Aga Khan, Herbert Swai, alisisitiza Watanzania kutumia fursa ya kuwezeshwa kupata matibabu ya afya kwa wakati.

Swai alisema kampuni hiyo ni mdau wa matibabu ya afya nchini ambayo husaidia kuwatafutia watu matibabu ya haraka ndani na nje ya nchi na wengi wamenufaika kwa kupata fursa ya matibabu katika nchi mbalimbali kama Uturuki, Uingereza, India na Afrika Kusini.

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED NA HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya notisi/Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | TAREHE NA SAA YA MNADA | MAHALI DHAMANA ILIPO | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MARRY AFANDE MWAIPOPO | MARRY AFANDE MWAIPOPO | NYUMBA YENYE LESENI YA MKAZI NA. TMK012270 | 27/03/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAKANGARAWE MANISPAA YA TEMEKE | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 2 | EDWARD E, MWAITENDA | EDWARD E, MWAITENDA | NYUMBA-HATI YA MAUZIANO | 25/03/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAPINGA MIANZINI, WILAYA YA BAGAMOYO | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 3 | EGBERT TRIPHON NGOZI | EGBERT TRIPHON NGOZI | NYUMBA – HATI YA MAUZIANO | 30/03/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MISEWE MTAA WA LIWITI, MANISPAA YA ILALA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 4 | EGBERT TRIPHON NGOZI | ELIAS RWEZAULA BULAYA | NYUMBA TITLE NA. 100988 MBA | 04/04/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TABATA MANISPAA YA ILALA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 5 | ANNA J, ISACK | SALUM IBRAHIM MAGIMBA | NYUMBA LESENI YA MAKAZI NA. TMK046320. PARCEL NA. TMK/MKW/YDV19/259 | 13/04/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | YOMBO DOVYA MANISPAA YA TEMEKE | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 6 | ANNA J, ISACK | MTUNDA RAMADHANI SELEMANI | NYUMBA –HATI YA MAUZIANO | 16/04/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | KIBONDE MAJI MCHIKICHINI MANISPAA YA TEMEKE | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 7 | CHARLES YUSUPH PUKA | CHARLES YUSUPH PUKA | NYUMBA – HATI YA MAUZIANO | 20/04/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MJI MPYA MAJOHE MANISPAA YA ILALA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 8 | CHARLES YUSUPH PUKA | GASPAR WILLIAM MWAKANYAMALE | NYUMBA YENYE HATI NA. 90710 PLOT.NA.635 | 24/04/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | PUGU MWAKANGA MANINSPAA YA ILALA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 8 | ALEX MTUNDU MHUMHA | ALEX MTUNDU MHUMHA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. ILA026481 | 02/5/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | KIPUNGUNI 'B' KITUNDA ILALA. | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 9. | COCO RIKO ENTERTAINMENT COMPANY LIMITED | JOHN CLARET MDENYE | 1. NYUMBA YENYE HATI NA. 778, PLOT NO. 528<br>2. NYUMBA YENYE HATI na. 781,PLOT NO 526,<br>3. ENEO LENYE HATI NA.20016, SHAMBA NA. 1853 | 25/03/2024, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | 1. OLASITI ARUSHA, PLOT NO 528,BLOCK A<br>2. OLASITI ARUSHA PLOT NO 526,BLOCK A<br>3. OLASITI VILLAGE, FARM NO 1853 | **HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali iliyopo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyo fikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne(14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki(transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na benki(eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | |
|---|---|
| **TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**<br>**P.O.BOX 1305, Songea,Ruvuma**<br>**Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298/ 0784 718 734**<br>**Email:twinscoltd5@gmail. com** | **HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**<br>**P.o.Box 11898, Arusha**<br>**Tel: 0784 200283/ 0767529605**<br>**Email: harvestercapital558@gmail.com** |

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Kila la kheri wawakilishi wetu michuano All African Games*

**MICHEZO** maarufu barani Afrika (All African Games) kwa mwaka huu imepangwa kufanyika katika jiji la Accra, Ghana na tayari imeshafunguliwa rasmi nchini humo.

Wanamichezo kutoka katika mataifa mbalimbali wako Ghana kwa ajili ya kupeperusha bendera za nchi zao kwenye michuano hiyo ambayo hushirikisha michezo ya aina mbalimbali.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingine, pia imepeleka wanamichezo wake katika mashindano hayo, ambao walipata tiketi ya kushiriki kwa mujibu wa kanuni zilizoandaliwa.

Kwa mara ya kwanza Tanzania imepeleka wanamichezo 75, ni rekodi ambayo haijawahi kuweka miaka iliyopita na hii inatokana na juhudi za nguvu zinazoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, za kusaidia kuanzia maandalizi na mahitaji mengine muhimu ya wachezaji ili kufikia malengo.

Tanzania imepeleka wachezaji wa mpira wa miguu wa wanawake (Tanzanite), judo, kriketi, riadha, kuogelea, ngumi, na waendesha baiskeli.

Kupeleka idadi hiyo ya wanamichezo si jambo la kukurupuka, hii imetokana na maandalizi sahihi yaliyofanywa na viongozi wa vyama husika kwa kuhakikisha wachezaji wanafikia vigezo vya kushiriki michuano hiyo, lakini pia kwa kuwapa motisha na kuwaamini wanaweza kubadilisha heshima ya Tanzania katika ngazi ya kimataifa.

Mapema wiki hii, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, aliikabidhi timu hiyo ya Tanzania bendera na wanamichezo hao kuwataka kwenda katika mashindano hayo kupambana ili kuipa heshima nchi yetu.

Ndumbaro alisema anaamini maandalizi waliyofanya yamewasaidia kuwaweka tayari na mashindano hayo huku akiwakumbusha wanakwenda katika michuano hiyo kama wawakilishi wa nchi na si vinginevyo.

Waziri huyo amewataka wanamichezo hao kujituma na kuonyesha viwango vya juu ili kurejea nyumbani na medali lakini pia kwenda kujifunza mbinu ambazo zinatumiwa na mataifa mengine ili kuibuka washindi, lakini pia kujihakikisha nafasi ya kufuzu mara kwa mara.

Kama ambavyo mwaka juzi Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 maarufu kwa jina la Serengeti Girls tumeishuhudia ikifuzu na kufika hatua ya robo fainali katika mashindano ya Kombe la Dunia yaliyofanyika India, tunaamini pia mwaka huu Tanzania itarejea na medali kutoka All African Games.

Medali ndio jambo pekee ambalo Tanzania inahitaji kupata baada ya wanamichezo wake kwa muda mrefu kuonekana wanakwenda kushiriki na si kushindana katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, umefika wakati nchi inahitaji kuona wawakilishi wake wanarudi na makombe na si kurejea wakiwa vichwa chini.

Lakini wakati wanamichezo hawa ambao leo karata ya kwanza itatupwa na Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite) ambao watakutana na majirani Uganda, timu hizo zikiwa Kundi A, wachezaji wengine waliobakia nyumbani wanatakiwa kujipanga ili kuhakikisha pia wanapata nafasi ya kushiriki katika mashindano mengine yanayofuata.

Tunawakumbusha wanamichezo kuandaliwa mapema, ni moja ya silaha kubwa ya kurejea nyumbani na medali, kwa sababu nchi inakuwa imepeleka wawakilishi ambao wameandaliwa vyema na wenye uzoefu unaotokana na kushiriki mashindano mengine mbalimbali.

Ikumbukwe mataifa yote ambayo yamekuwa yakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, msingi wa matokeo hayo chanya hutokana na wanamichezo wake kuandaliwa mapema na si kufanya maandalizi ya zimamoto.

Kila la kheri wanamichezo wote wa Tanzania wanaopeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya All African Games.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






# Muungwana Lazima Nilonge

## *Michezo ya Kubeti itambulike ni burudani na isigeuzwe ajira*

Na Joseph Mwendapole

**HIVI** karibuni Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Nchini (GMT), ilifanya mkutano wa kawaida na waandishi wa habari na wahariri kuelezea shughuli zake ili umma ufahamu kwa mapana kuhusu maana ya michezo ya kubahatisha.

Bodi hiyo ambayo ilianzishwa miaka 20 iliyopita imekuwa ikifanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria za Tanzania kwa kudhibiti shughuli za kubahatisha zisifanyike kiholela.

Shughuli za kubahatisha zimekuwa vyanzo vikubwa vya mapato kwa serikali licha ya baadhi ya watu kuwa na mtazamo hasi kuhusu shughuli za kubahatisha.

Lakini pamoja na yote hayo bodi imekuwa ikifanya shughuli zake huku ikionya na kutoa elimu hasa vijana kuhusu michezo ya kubahatisha siyo mbadala wa ajira na badala yake baadhi ya watu huitumia kama burudani.

Bodi hiyo inasema vijana wanapaswa kutafuta shughuli za kuwaingizia fedha na watumie michezo hiyo kama sehemu ya burudani badala ya kuigeuza kuwa chanzo chao cha mapato.

Baadhi ya watu wamekuwa na mtazamo hasi kuhusu michezo ya kubahatisha wakijenga hoja imeteka uraibu kwa vijana wengi kiasi cha kushindwa kufanyakazi rasmi na kushinda kwenye vibanda vya michezo hiyo.

Wapo ambao wamekuwa wakilitazama hilo kwa msingi wa imani zao na kuna wengine wamekuwa wakilitizama kwa jicho la jamii kwamba mwisho wa siku uraibu wake unaweza kuleta shida katika kizazi kijacho.

Lakini tunapaswa kujua GBT ilianzishwa kwa ajili ya kudhibiti uraibu, kukiukwa kwa taratibu za michezo hiyo hivyo hasara za kutokuwapo kabisa kwa bodi ni kubwa zaidi kuliko kuiacha ikaendelea kutimiza wajibu wake.

Licha ya hoja zote michezo hiyo imekuwa chanzo cha mapato ambao husaidia mapato ya serikali mwaka hadi mwaka, na kwa mfano kodi inayopatikana kwa mapato hayo iliongezeka kutoka Sh. bilioni 33 kwa mwaka 2017, hadi Sh. bilioni 170 hapo mwaka jana, pato ambalo ni wastani wa ongezeko la asilimia 407.

Kuanzishwa kwa bodi hiyo kulisababisha sekta ya michezo ya kubahatisha kuratibiwa vizuri na hivyo kuwa moja ya shughuli muhimu na rasmi katika uchumi wa nchi na chanzo muhimu cha mapato ikiwa ni pamoja na kuchangia kukuza ajira nchini.

Sekta hiyo imekuwa ikikua kwa kasi kiasi cha kuhitajika kwa udhibiti ulio imara wenye kushirikisha wadau mbalimbali ikiwamo wanahabari ili kuleta matokeo chanya zaidi ya kiuchumi na kijamii.

Sekta hii licha ni ya burudani lakini ni ya biashara kwa waendeshaji hivyo ni sekta ya kiuchumi pamoja na burudani kwa taifa kwa ujumla na dhana kuu katika sekta hiyo ni bahati hivyo washindi hupatikana kwa bahati tu na si vinginevyo.

James Mbalwe ambaye ni Mkurugenzi wa GBT, anasema mshindi anapata vitu viwili katika mchezo huu, anaweza kupata burudani na vile vile zawadi iwapo ataibuka mshindi na sekta hiyo imefanikiwa kuzalisha ajira 25,000.

Anasema michezo ya kubahatisha inahusisha kasino, mashine za sloti, ubashiri wa matokeo ya michezo, bahati nasibu ya jumbe fupi za simu, bahati nasibu ya taifa .

Anasema majukumu mengine ya bodi ni kushauri kuhusu namba ambavyo serikali inavyoweza kukusanya kodi na tozo zingine katika sekta ya michezo ya kibiashara.

Anasema kifungu cha saba cha sheria kinawapa mamlaka ya kutoa leseni ya kubahatisha pamoja na kusitisha pale mhusika anapofanya mambo yanayokwenda kinyume na leseni yake.

Anasema mchakato wa kutoa leseni unahusisha uchunguzi wa kina wa tabia za mwomba leseni na uchunguzi huwa unahusisha kama mhusika ana historia ya uhalifu na kujua vyanzo vyake vya fedha.

Anasema wanachunguza pia uwezo wa mwombaji kifedha na kiteknolojia na pia washirika wake pamoja na kuangalia uadlifu wao katika kufuata sheria za nchi.

Anasema mageuzi ya kiuchumi yaliyotokea nchini kuanzia miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa mwaka 2000 ambayo yaliwezesha kuanzishwa kwa biashara huria hayakuiacha nyuma sekta ya biashara ya michezo ya kubahatisha kwani nayo ilianzia hapo.

Anasema kupitia mageuzi hayo sekta hiyo ilipitia katika mabadiliko makubwa ambapo mwaka 2000 Sera ya Taifa ya Michezo ya kubahatisha ilitungwa ambayo ilitaka kuwepo kwa mamlaka ya kudhibiti michezo hiyo.

Aliongeza lengo la kuanzishwa kwa GBT ni kuwezesha sekta hiyo kuchangia ipasavyo kwenye pato la taifa huku ikilinda maslahi na ustawi wa jamii kwa ujumla.

# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI KATIKA PICHA




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, akiwahutubia wananchi kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Dumiani, wilayani Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Wanawake wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wakiwa kwenye maandamano katika barabara ya Samora, jijini Dar as Salaam jana, wakiadhimisha Kilele cha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wafanyakazi wa BRAC kutoka Makao Makuu ya Shirika hilo wakikabidhi msaada wa chakula na vifaa vya usafi kwa wanafunzi wa Shule ya Wasichana ya Bethsaida ya Mpiji Magohe, Dar es Salaam jana, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Dereva mwanamke akiwapungia kwa bendera kinamama (hawapo pichani), waliokuwa wakiandamana katika kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, wilayani Chamwino jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa (wa pili kushoto), akiwa na Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri (kushoto), wakitembelea maonyesho ya Wanawake Wajasiriamali 2024', katika viwanja vya ubalozi huo, jijini Dar es Salaam jana, kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**



Wanawake wa Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI) wakiwa na vitu mbalimbali kabla ya kutoa msaada wa dawa na mahitaji muhimu kwa wagonjwa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road jijini Dar es Salaam jana, kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viwanja 10,000 kupimwa wanaohama Ngorongoro

**Na Munir Shemweta,** MSOMERA

VIWANJA 10,000 vinatarajiwa kupangwa na kupimwa katika eneo lililokuwa pori tengefu la Handeni awamu ya pili kwa ajili ya wakazi wanaohamia kutoka Hifadhi ya Ngorongoro.

Hayo yalibainishwa juzi na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, katika eneo linalotekelezwa mradi wa kupima viwanja na mashamba wakati wa ziara ya pamoja ya mawaziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na ile ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenye eneo la kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga.

Naibu Waziri Pinda alisema kati ya viwanja hivyo, 5,000 ni kwa ajili ya makazi na 5,000 ni mashamba.

Kwa mujibu wa Pinda, viwanja 2,500 vya makazi vitapimwa kwenye kijiji cha Msomera, 1,500 kijiji cha Kitwai B (Simanjiro) na 1,000 kijiji cha Sauyi (Kilindi).

Alisema hadi kufikia Februari 28, mwaka huu, viwanja 5,882 vilikuwa vimepimwa sawa na asilimia 118 ya lengo la kupima viwanja 5,000 katika maeneo ya upangaji ya vijiji vya Saunyi na Msomera.

Pinda alibainisha kuwa kati ya viwanja hivyo, 5,272 ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi pekee, hivyo kuwa na ziada ya viwanja 610 ikilinganishwa na malengo ya upatikanaji viwanja 5,000.

Naibu Waziri aliweka wazi kuwa upimaji mashamba unaendelea katika kijiji cha Msomera na hadi Februari 28, mwaka huu, mashamba 3,507 yalikuwa yamepimwa sawa na asilimia 70 ya lengo la kupima mashamba 5,000 katika maeneo ya upangaji ya Msomera, Saunyi na Kitwai.

"Ili kufikisha lengo la kupima mashamba yaliyobaki 1,493 tunategemea kukamilika kazi ya uwandani ndani ya wiki mbili, kazi ya uandaaji wa mipangokina kwa ajili ya upimaji mashamba inaendelea," alisema.

Pinda alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi vifaa alivyosema vimesaidia na vinaendelea kusaidia katika utekelezaji wa mradi katika kijiji cha Msomera na maeneo mengine.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kufanikisha mipangpo kina na hatimaye kupima mashamba na viwanja katika eneo la Msomera.

"Kazi imeonekana na tumeona kazi nzuri ambayo imekwisha kuanza na inaendelea ya upimaji viwanja na mashamba katika maeneo ya kilimo na mifugo katika eneo hili la Msomera," alisema.

Utekelezaji wa mradi wa kupanga na kupima eneo la Msomera umefanikisha kuwaweka pamoja wageni wanaohamia kwa hiari kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na wenyeji waliokutwa kwenye eneo la pori tengefu kuisha pamoja na pasipo migogoro yoyote.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (katikati), akiongoza kikao cha Bodi ya Barabara, mjini Musoma mapema wiki hii, kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuboresha miundombinu ya barabara mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji China wamiminika kusaka fursa

**Na Joseph Mwendapole**

UJUMBE wa wawekezaji 100 kutoka China uko nchini kwa ajili ya kutafuta fursa mbalimbali za uwekezaji na maeneo ya kuingia ubia na wafanyabiashara wa Tanzania.

Wawekezaji hao juzi walifanya mkutano na wenzao wa Tanzania ulioratibiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na kuonyeshwa fursa zilizopo nchini.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mkurugenzi wa Huduma za Uwekezaji wa TIC, Mafutah Bunini, alisema mazingira ya uwekezaji yamewavutia wafanyabiashara wengi wa China na idadi yao inatarajiwa kuongezeka maradufu.

Alisema kwa miaka mingi China ndiyo inaongoza kwa uwekezaji mkubwa nchini ambapo tangu TIC ianze kusajili miradi, tayari miradi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 11 imeshasajiliwa.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha wafanyabiashara hao wa China na Watanzania ili kubadilishana mawazo na maeneo ambayo wanaweza kufanya uwekezaji kwa ubia.

Alisema kwenye kongamano hilo amezungumza na Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara wa China ambaye amemhakikishia kuwa hivi karibuni kundi kubwa lingine la wafanyabiashara kutoka nchini humo watakuja kutafuta fursa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA), Charles Itembe, alisema ujumbe huo wa wafanyabiashara ni ishara kwamba serikali imefanya uhamasishaji mkubwa wa kuvutia uwekezaji mpya kutoka nje ya nchi.

Alisema tangu EPZA ianzishwe kampuni 35 zimewekeza kwenye eneo hilo kiasi cha Dola za Marekani milioni mbili katika sekta ya madini, kuongezea thamani bidhaa na uchakataji wa mazao mbalimbali.

"Ujio wa wawekezaji unaendelea kuwa mkubwa sana hasa kwenye siku za hivi karibuni na imechangiwa na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo na tumepata kampuni nyingi sana za China zinaonyesha nia ya kutaka kuja kuwekeza," alisema.

Alisema kampuni zilizowekeza kwenye ukanda wa EPZA umesababishisha ajira 20,000 za moja kwa moja na kuongeza kuwa kuna haja serikali ikaendelea kuweka vivutio vya uwekezaji ili kuwavutia wengi.

Alisema bidhaa za Tanzania zinafursa kubwa ya masoko nchini Marekani kupitia soko la AGOA na kwamba hivi karibuni Uingereza nayo itaanza kuruhusu bidhaa za hapa nchini kuingia kwenye masoko yake bila kutozwa ushuru. "Tuna pia fursa ya masoko ukanda wa Afrika Mashariki ambapo iwapo tutaitumia vizuri fursa iliyopo ya kufanyabiashara kwa ubia na hawa wachina tutauza bidhaa nyingi nje ya nchi na tutapata fedha nyingi za kigeni," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara wa China, Feng Zhenyu, alisema wafanyabiashara wa China wamevutiwa na mazingira ya uwekezaji na ndiyo sababu wamekuja kwa wingi kutafursa fursa za kuwekea na hata zile za ubia. Alisema Tanzania na China zimekuwa na uhusiano mzuri wa kidiplomasia kwa muda mrefu hali ambayo imesaidia wafanyabiashara wa mataifa hayo kuwa rafiki na kufanya biashara mbalimbali.

"Tumeona fursa nyingi hapa Tanzania na kwa mfano tu kwenye sekta ya kilimo, madini kuna fursa nyingi kwa hiyo tumeona tukutane na taasisi za serikali na wafanyabiashara tuone namna ya kuwekeza," alisema.

Alisema hata kituo cha kuhudumia wawekezaji sehemu moja kilichoanzishwa na TIC kimekuwa kivutio kikubwa kwani mwekezaji anaweza kusajili mradi akiwa nchi yoyote duniani.

# Walia uhalifu kuota mizizi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa, wamelalamikia kuongezeka kwa matukio ya uporaji, kujeruhi, ubakaji na mauaji wakihusisha na changamoto ya kutokuwapo kwa taa za barabarani.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii jana walisema kadri siku zinavyokwenda hali ya usalama inazidi kupungua na wananchi wanapatwa na hofu kwa kuwa hawajui hatima yao.

Mkazi wa eneo hilo, Paul Songa, alisema kuwa yapo baadhi ya mambo yanayochangia ikiwamo kukosekana kwa taa za barabarani nyakati za usiku.

"Wananchi wamekuwa wakitembea baadhi ya maeneo kukiwa na giza totoro, hali inayotoa mwanya kwa watu waovu kufanya vitendo vya uhalifu kwao," alisema.

Songa alisema kuwa imezoeleka katika mji huo kuona taa za barabarani zikiwaka usiku wakati kukiwa na ziara ya kiongozi wa kitaifa hasa ziara ya Rais, Makamu wa Rais au Waziri Mkuu, tofauti na hapo ni giza.

"Hata tusiposikiliza vyombo vya habari, ili kujua kama kuna ziara ya kiongozi wa kitaifa anakuja katika mji huu, tukiona taa za barabarani zinawaka tunajua tu tayari anakuja kiongozi wa kitaifa.

"Wamemwashia taa ili asipite kwenye giza, lakini manispaa hawana muda kabisa na sisi (wananchi)," alidai.

Mkazi mwingine, Macrina Kulawaya, alisema changamoto nyingine ni maeneo ambayo yanamilikiwa na serikali au taasisi zake ambayo ni viwanja ambavyo havijajengwa.

"Havifanyiwi usafi kama kupalilia au kufyeka majani matokeo yake kunageuka kuwa vichaka vya kujificha watu waovu na wavuta bangi.

"Katika maeneo hayo nyakati za usiku wanawake wamekuwa wakikabwa, wakiporwa fedha na vitu vingine, vyenye thamani, kupigwa na hata kubakwa," alisema.

Fraviana Kamalamo, alisema polisi mjini Sumbawanga wamekuwa wakifanya doria za mara kwa mara baadhi ya maeneo, lakini kutokana na uchache wao hawawezi kuwapo kila sehemu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Catherine Mashala, alikiri kuwapo kwa changamoto hizo na kueleza mikakati yao.

Alisema katika maeneo ambayo ni vichaka na yanamilikiwa na serikali hasa yake yaliyo karibu na nyumba ya Mkuu wa Wilaya, halmashauri itawasiliana na magereza ili wafungwa wakafanye usafi haraka kukabiliana na hali hiyo.

Kuhusu changamoto ya taa za barabarani, Catherine alisema halmashauri kupitia Baraza la Madiwani tayari limeshatenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2024/25 kwa ajili ya kuweka taa za sola.

Pia alisema tayari wamewasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ili kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) usaidie kuweka taa hizo.





# Wanawake wafundwa mikopo kausha damu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WIZARA ya Fedha imetumia wiki ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kutoa elimu ya kifedha ili kuwasaidia kujiepusha na mikopo umiza na nyonya damu.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Fauzia Nombo, aliyasema hayo juzi kwenye ufunguzi wa maonyesho ya maadhimisho ya siku hiyo yanayofanyika kiwanja cha Mashujaa jijini hapa ambayo yalifunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule.

Alisema wanawake wengi wamekuwa wakiingia kwenye mikopo hiyo kutokana na kukosa elimu ya kifedha ambayo kusababisha kupoteza mali zao kwa kushindwa kulipa mikopo hiyo.

Alibainisha kuwa watumishi wa wizara hiyo wapo kwenye banda la wizara hiyo kwa kuwasaidia wanawake hao kupata elimu ya kifedha kwa ujumla kuanzia mikopo na jinsi ya kutunza fedha zao.

Nombo alisema wizara hiyo itatumia maonyesho hayo kutoa elimu kwa wanawake kuhusu utunzaji wa fedha pamoja na kujiandaa kuelekea uzeeni.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa (UN WOMEN), Sizarina Hamisi, alisema shirika hilo limekuwa likishirikiana na serikali katika kuhakikisha wanasukuma haki za wanawake kuzingatiwa na kuwajengea uwezo wa uongozi katika nafasi za kisiasa na kiserikali.

Akifungua maonyesho hayo, Senyamule aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi ili kupata huduma za elimu ya haki zao mbalimbali ambazo zinatolewa na taasisi za serikali na binafsi kwenye maonesho hayo.

## Samia kuteta na wanawake nishati safi ya kupikia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuzungumza na wanawake kuhusu nishati safi ya kupikia kupitia kongamano la wanawake linalofanyika jijini Dodoma.

Kongamano hilo ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

Akizungumza kuhusu kongamano hilo, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema watashiriki wanawake zaidi ya 4,000.

"Niwaalike wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma kushiriki kongamano hili, takwimu zinaonesha takribani asilimia 63 ya Watanzania wanatumia kuni kupikia na asilimia 25 wanatumia mkaa na asilimia tano wanatumia nishati mbadala ikiwamo gesi," alisema.

Alieleza kuwa bado kuna safari ndefu kufikia matumizi ya nishati safi ya kupikia na wanaamini ifikapo mwaka 2033 azma ya Rais itatimia ya kuhakikisha Watanzania wanatumia nishati hiyo.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akimsikiliza Ofisa wa Dawati la Wanawake Wizara ya Fedha, Wapheba Settembo (kushoto), alipotembelea banda la wizara hiyo kwenye maonyesho ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani katika viwanja vya Mashujaa, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DIT na Tengeru kusaidia sera za kuinua wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imesema itashirikiana na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii ya Tengeru kusaidia serikali kutunga sera na sheria zinazoweza kuwainua wanawake kiuchumi na katika fursa mbalimbali.

Mwakilishi wa DIT, Dk. Daud Simbeye, aliyasema hayo jana kwenye kongamano la wanawake lililoandaliwa na taasisi hizo kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Alisema taasisi hizo zinatambua mchango wa mwanamke na kuthamini jitihada zake katika kuleta mafanikio na kuhamasisha mabadiliko ya jamii kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

Naye Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dk. Bakari George, alisema kupitia Kituo cha Kitaifa cha Utafiti na Machapisho Yahusuyo Wanawake (NWRDC) kwa miaka mitatu sasa imekuwa ikiandaa kongamano ili kujadili utafiti na masuala kadhaa ya wanawake.

"Kongamano hili linakusudia kujadili tafiti zipatazo 12 na maandiko ya mawazo bunifu manne yaliyofanywa na wanataaluma na mashirika mbalimbali kuhusu masuala ya kijinsia, tunashirikiana kikamilifu katika kutatua changamoto za wanawake na jamii sisi Tengeru tutaibua na wenzetu DIT watatumia teknolojia kutatua," alisema.

Awali, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Josephine Mwaipopo, alishukuru taasisi hizo mbili kwa kuona Dodoma ni sehemu sahihi ya kufanyia kongamano hilo kwa kuwa itakua ni chachu kwa wanawake wa Mkoa wa Dodoma kuamka na kujipambania kiuchumi na kuimarisha vipato vya familia zao.



# Hemed ataka viwango ujenzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleima Abdulla, amewasisitiza makandarasi na wasimamizi wa ujenzi wa mtaro wa dharura unaojengwa katika eneo la Kibonde Mzungu, kuhakikisha unajengwa kwa viwango vilivyokusudiwa ili kuyawezesha maji kupita vizuri na kuwaondolea kero wananchi.

Hemed alisema hayo jana katika ziara yake ya kukagua maendeleo ya uchimbaji wa mtaro huo pamoja na kuangalia bwawa linalotuwama maji ya mvua lililoko Fuoni Jangamizi, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja.

Alisema serikali itaendelelea kutatua changamoto zinazowakabili wananchi wake na kumalizika kwa mtaro huo kutasaidia kuondoa tatizo la kutuwama kwa maji ya mvua katika eneo hilo na maeneo jirani yanayosababisha wananchi kuhama sehemu makazi hasa wakati wa mvua za masika.

Hemed alisema taasisi husika ni lazima kuongeza kasi katika uchimbaji wa mtaro huo ili kukamilika kabla ya mvua za masika kuanza na kuahidi kuwa serikali itatoa ushirikiano wa hali ya juu ili kukamilisha ujenzi wa mradi huo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa.

Pia aliwataka wakazi wa maeneo hayo na ya jirani kutoa ushirikiano kwa serikali ili kusaidia mradi huo kukamilika kwa wakati sambamba na kufuata utaratibu utakaowekwa baada ya kukamilika kwa ujenzi.

Aidha, aliitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar (Zawa), Idara ya Mazingira na Kamisheni ya Kupambana na Maafa kukaa na wananchi wa Shehia ya Fuoni Chunga ili kulitafutia ufumbuzi tatizo la kutuama kwa maji katika eneo la Fuoni Jangamizi ambalo ni kero kwa wakaazi na kuwa na hofu ya kutokea maafa.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Hamza Hassan Juma, alisema tayari wataalamu wa kufanya upembuzi yakinifu wameshafika Kibonde Mzungu kuangalia jinsi ya kuwatatulia wananchi changamoto hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa maeneo hayo, Dk. Zaharan Nassor aliishukuru serikali kwa kuwachimbia mtaro huo ambao utatatua tatizo la kutuama kwa maji maeneo hayo ambayo yalikuwa yakiwasumbua kwa muda mrefu kila ifikapo wakati wa mvua kubwa.

# Wateule waahidi makubwa wakila viapo

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaapisha makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na mhasibu mkuu wa serikali aliowateuwa hivi karibuni katika hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya Ikulu, Zanzibar.

Katika uteuzi huo, Dk. Mwinyi amewabadilisha baadhi ya makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu kutoka wizara moja kwenda nyingine, huku akiendelea kuwapa nafasi zaidi wanawake.

Wakizungumza jana baada ya hafla hiyo, viongozi hao walioapishwa walisema watafanya kazi kwa uadilifu na bidii katika kuwatumikia wananchi kwa maslahi ya taifa. Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Khadija Khamis Rajab, alisema wananchi wategemee mabadiliko makubwa katika utendaji kazi wa wizara hiyo ambayo nafasi za juu ikiwamo ya waziri, naibu waziri na katibu mkuu unaongozwa na wanawake.

"Nitahakikisha nafanya kazi kwa ushirikiano na watendaji wezangu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na wananchi watarajie mabadiliko makubwa ya maendeleo hasa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi," alisema.

Aboud Suleiman Jumbe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, alisema atatekeleza vipaumbele vya serikali kutokana na utalii kuwa sekta mama ya sera ya uchumi wa buluu. Asilimia 32 ya pato la taifa Zanzibar linatokana na sekta ya utalii.

Maeneo mbalimbali, alisema yanahitaji kuimarishwa na kuongezewa vipaumbele ikiwamo utalii kwa wote, utalii shirikishi na unaozingatia masuala ya usalama wa wananchi na watalii, unaojali ubunifu, nyenzo na unaobadilisha sekta ya mikutano ya kimataifa, afya na michezo.

Alisema atatekeleza vipaumbele hivyo ili kuendana na ushindani wa utalii wa kimataifa na kuongeza nyenzo, misingi, uwekezaji na kuvutia sera mbalimbali ambazo zitaimarisha na kupelekea soko la utalii kuzidi kuleta pato la taifa.

Naye Mhasibu Mkuu wa Serikali, Hamad Saleh Hamad, alisema atafanya kazi kwa uadilifu ili kupeleka mbele maendeleo ya nchi na taaluma ya uhasibu inaongozwa na maadili na haziruhusu kufanya masuala ya wizi wala ya ubadhirifu wa fedha za umma.



Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (SMZ), Siti Abass Ali (kulia), akizungumza alipofungua mafunzo ya kutumia mikopo ya benki kwa wajasiriamali wa Mkoa wa Mjini Magharibi juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar yajivunia wanawake kupaa katika uchumi, uwekezaji na uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema wakati dunia inaadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Zanzibar kuna mabadiliko ya uwekezaji kwa wanawake katika sekta ya uchumi, teknolojia, viwanda na kisiasa.

Pembe aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo ambayo hufanyika Machi 8 kila mwaka duniani.

Alisema uwekezaji katika siasa unakua siku hadi siku kwa kuwapo kwa ustawi wa kisiasa, hivyo kuimarisha demokrasia na ushiriki wa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi.

"Tumeshuhudia katika serikali ya awamu ya nane, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameongeza nafasi kwa wanawake katika ngazi mbalimbali wakiwamo mawaziri, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu, wakurugenzi, makamishna na majaji katika mahakama," alisema.

Waziri Pembe alisema uwekezaji huo ni ishara kubwa ukuaji wa demokrasia na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na malengo endelevu ya dunia (SDG). Pia alisema taasisi za utafiti zinaonyesha kwamba watumiaji na wawekezaji katika sekta ya kati ni wanawake ambao kwa kiasi wanatumia teknolojia katika uzalishaji mali na hata uwekaji wa mifumo kupitia program za afya, kilimo, uwekezaji katika sekta ya fedha, elimu na utambuzi ambazo walengwa wakubwa ni wanawake, wasichana, vijana na watoto.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2023/24 mamlaka za uwekezaji na taasisi za fedha zimewawezesha wanafaika 20,412 kwa kuapatia mikopo Unguja na Pemba na kati ya hao, wanaume ni 8,103 na wanawake 12,309 wakiwamo watu wenye ulemavu.

"Ni jumla ya Sh. 24,152,930,054 zimetolewa na mamlaka za uwezeshaji kiuchumi ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kujipima na kuwawezesha wanawake kufikia hali ya usawa wa kiuchumi na usawa wa kijinsia," alisema.

Waziri Pembe alizitaka taasisi na wadau kuzingatia umuhimu wa uwekezajii kwa wanawake katika nyanja za uchumi, kijamii na kisiasa ili kufikia wigo mpana wa maendeleo kwa sababu maeneo hayo yanaweza kuwa na mchango katika kubadili maisha ya wanawake.

"Pia taasisi ziweke mifumo bora ya matumizi ya teknolojia na ubunifu ili kukinga matumizi mabaya ya mifumo hiyo kwa maslahi ya taifa kwa kizazi cha leo na baadaye," alisema.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kupunguza na kukinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kufanya kazi kwa ufanisi, hivyo kuleta mabadiliko ya maisha kwa wanawake na wanaume.



KHADIJA KOPA

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI MACHI 9, 2024



# MBONA WAKO SAWA!

LICHA ya maneno mengi kuhusu uhalali wa uhusiano wao, staa wa Bongo Fleva, Rajab Abdul Kahali, maarufu Harmonize na mpenzi wake mpya Poshy Queen, wameonekana kuziba masikio wakiendelea kula maisha pamoja.

Uhusiano huo kati ya Harmnonize na Poshy Queen, uligubikwa na kelele kila upande kutokana na madai kuwa mwanamuziki huyo alimfanyia umafya rafiki yake na kumpora mwanamke huyo bila huruma.

Hata hivyo, wawili hao wameonekana kuweka pamba masikioni wakionekana wakila bata katika sehemu mbalimbali na kila mmoja akimsifia mwenzake kutokana na mahaba mazito wanayopeana.

Katika kuonyesha kwamba wao sasa ni kitu kimoja, wameamua kuwaweka pamoja watoto wao ambao wote ni mabinti kwa lengo la kuwalea kama familia moja.

Binti wa Harmonize anayeitwa Zuuh na Nova ambaye ni mtoto wa Poshy Queen, kwa sasa wanaishi katika jumba la kifahari la Konde Boy wakila na kucheza pamoja.

Katika video ambayo wapenzi hao walichapisha kwenye kurasa zao Ijumaa, walionekana watoto hao wakichora pamoja huku wakionyesha uhusiano mzuri kati yao.

"Tunawajibika rafiki yangu Poshy Queen  kheri ya siku ya kimataifa ya wanawake wasichana wangu," ameandika Harmonize katika ukurasa wake wa Instagram.

Baadhi ya watu wanaeleza Harmonize ametoa ujumbe mpana kwa watu wanaomfuatilia kwa kuwaonyesha kwamba kila kitu kwao kiko sawa na wameanza kujenga familia yao kwa pamoja.

BASI SAWA

## Brown aponda maisha ya Kenya



MSANII wa muziki kutoka Kenya, Otile Brown, amethibitisha kwamba maisha ya wasanii ndani ya nchi hiyo ni magumu kutokana na gharama kuwa juu kuliko nchi jirani ya Tanzania.

Katika mahojiano yake ya hivi karibuni, Brown, amesema kutokana na hali hiyo pesa anazozipata ndani ya nchi yake na kama akienda Tanzania ataishi maisha ya kifahari.

Brown alisema gharama ya kupanga nyumba nchini humo ni kubwa ukilinganisha na Tanzania na kwamba angeishi katika kasri kama la kifalme.

“Mimi pengine nyumba ambayo ninalipa kodi hapa Kenya, pesa hizo za kodi kama ningekuwa Tanzania ningekuwa naishi kwenye kasri,” amesema.

## Khadija Kopa asema ajali kazini



MALKIA wa taarab nchini ambaye ni mama mzazi wa Zuchu, amezungumzia suala la kupigwa marufuku kwa mwanawe kutumbuiza visiwani Zanzibar, kuwa ni tukio la ajali kazini.

Akizungumza katika kituo cha Wasafi, Kopa amesema kabla ya kutolewa adhabu hiyo, alikaa chini na mwanawe kumuonya tabia hiyo ambayo inaweza kumuweka pabaya kisanii.

“Kama wanavyosema ajali kazini, ndio ishakuwa. Yataisha, hakuna jambo lisilokuwa na mwisho. Nimempa moyo lakini na mimi nimemwambia kuna vitu vingine havifai. Yaani tuseme wakati mwingine mdomo wa mama unakuwa na nuksi fulani,” amesema Kopa.



# MWIJAKU ATETEA KUMLINDA MKEWE

MSANII wa filamu na mchekeshaji, Mwijaku, amesema hapendi mke wake kusafiri na amempa masharti endapo anataka kufanya hivyo.

Mwijaku amesema anajua mke wake ni mzuri na kuna baadhi ya wanaume wanamnyemelea na ndio maana amempiga marufuku kusafiri peke yake.

“Nampenda mke wangu, sitaki asafiri peke yake na hata mabosi wake nimewaambia jambo hilo, labda mimi mwenyewe niwepo ndio anaweza tukasafiri,” amesema.

FILAMU

# Kisasi cha utata mtupu

**Na Adam Fungamwango**

NDIYO unaweza kusema kisa cha utata. Ni utata tupu. Filamu inaitwa ‘Kisasi cha Utata.’ Inazungumzia mambo ya kishirikina yanayofanywa au kuaminiwa na baadhi ya watu ndani ya jamii.

Imechezwa na Glori Isack, Mkali Makali, Careen Salvius, Huzuni, bibi Careen, Mkosa Sura Eliza.

Kwenye kijiji kimoja hapa nchini wananchi walikuwa wanapotea na wengine kukutwa wamekufa bila sababu yoyote.

Hali hiyo inasababisha Mwenyekiti wa Kijiji kuitisha kikao ili kutafuta ufumbuzi ya tatizo linalowakabili.

Hata hivyo kikao kinavunjika bila muafaka wowote, kwani kuna baadhi ya wanakijiji walipendekeza waletwe mganga wa kienyeji kutoka vijiji vya mbali ili kuangalia tatizo ni nini, lakini wengine walikuwa wanapinga katakata.

Katika kijiji hicho, bi Huzuni akiongoza kikundi cha watu washirikina, ambao kazi yao kijijini hapo ni kuwatia watu hofu, wakishindwa kufanya maendeleo au kulima kilimo chenye tija kwa kuhofia kurogwa.

Moja kati ya masharti ya chama hicho cha giza, ni kutoa watoto wao kafara kila mwaka.

Katika mkutano wao mmoja wa wanachama analalamika kuwa yeye kila mwaka anatoa mtoto wake na sasa amebaki mmoja tu.

Ni baada ya kuambiwa mwaka huu anatakiwa amtoe kijana wake katika kafara lao la kila msimu.

Siku zinapita aliyetakiwa kutoa kafara kijana wake hajafanya hivyo. bi Huzuni anamfuata nyumbani kwake na kumuuliza.

Dada wa kijana huyo anasikia maongezi hayo. Hapo sasa anathibitisha kuwa mama yao ni mshirikina.

Anakwenda kumwambia kaka yake, na hapo hapo anamshauri waondoke kijiji hapo kwenda kwa mganga wa kienyeji ili kuzuia mpango huo. Njiani wakakutana na mauzauza ya watu ambao hawaeleweki wanaoziba njia na kulazimika kukimbia kurudi nyumbani.

Mwenyekiti naye alikumbana na matokeo kama hayo alipokuwa akihangaika kutafuta suluhu.

Mwisho wa siku alifanikiwa. Aliletwa ‘mtaalam’ ambaye aliwaumbua washirikina wote kijijini hapo waliokuwa wakiongozwa kwa bi Huzuni.

Wanakijiji walichachamaa wawachome moto wote, lakini mganga anawaombea msamaha na wenyewe wakaomba msamaha, uchawi wao unachomwa moto, amani ikarejea kijijini.







# Sholo Mwamba awapa makavu

MWANAMUZIKI mkongwe wa Sengeli nchini, Sholo Mwamba, amesema baadhi ya wasanii wana chuki binafsi kiasi cha kumzibia asitumbuize katika shughuli za kiserikali.

Amesema kuwa wasanii wengi wa muziki huo yeye ndiye amewainua na kufika mbali, lakini kwa sasa wamebadilika baada ya kupata mafanikio.

“Baadhi ya wasanii wana chuki binafsi, hawapendi kuona natumbuiza katika mikutano ya kiserikali, wanaeneza mambo yasiyo na maana kwa kuwa tu nina mwonekano wa uswahilini,” amesema Sholo Mwamba.

## WANAUME HAPA WAMEPIGWA!

**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi wanaume huwafanyia visa vingi wapenzi na wake zao, lakini wakifanyiwa wao wanalalamika sana.

Nyimbo kama ‘Karubandika’ na ‘Mayanga’ zote za Maquiz Original, ‘Pendo’ wa Bima Lee, ‘Homa Imenizidia’ wa Orchestra Safari Sound ya mtindo wa Ndekule, na ‘Karumanzira’ wa Juwata Jazz msondo Ngoma, zote hizi tunaona mwanaume wakiwadanganya wanawake, wengine wakiwatoa vijijini na kuwaleta mjini wakidai ni maofisa, wakitaka waachike kwa waume zao ili wawaoe, lakini kumbe ni ulaghai tu badala yake wamewaingia chaka.

Zipo nyimbo ambazo wanawake bao wanajibu mapigo kwa wanaume, na sikia wanavyolalamika.

**Milima ya Kwetu-Super Rainbow**

Wimbo huu ni wa mwanzoni mwa miaka ya 1980, ulitungwa na marehemu Eddy Sheggy akiwa na Super Rainbow. Unamzungumzia mwanaume anayelalamika kumtoa mwanamke kijiji na kumleta mjini. Bibie akabadilika, kila kitu kakijua. Akageuka yeye ndiyo mtoto wa mjini. Akaanza kumfanyia vituko mumewe, mwishowe akamkimbia kabisa.

Bwana anarudi kwao Tanga yupo ndani ya basi anawaza akirudi atasema nini, maana alimuoa kwa harusi ya kifahari, walitoka wawili, leo anarudi peke yake.

**Solemba-Juwata Jazz Band**

Katika ya miaka ya 1980, marehemu Nico Zengekala akiwa na Juwata Jazz Banda alitunga wimbo wa ‘Solemba’ Maudhui yake ni jamaa aliyelalamika kuwa aliahidiwa na mwanamke mmoja aende nyumbani kwake baada ya kuelewana kimapenzi. Lakini alichokikuta huko ni simulizi.

Yalikuwa ni matusi na dharau, na demu akadai kuwa hamfahamu huyo kijana, badala yake anamsumbua bure, hana mpango wake. Bwana limemshuka.

**Shahada wa Uvumilivu-DDC Mlimani Park**

Ni kisa cha kusikitisa, cha jamaa mmoja aliyechukuliwa mke na jamaa mmoja ambaye alimwahidi kumjengea nyumba. Mke akamkimbia kwenda kwa huyo hasidi. Sasa katika wimbo huu rafiki zake wanamwita aende Sikinde Ngoma ya Ukae wakamtunukie shahada wa uvumilivu, kwani pamoja na maumivu, lakini hakutaka kulipiza kisasi.

**Nimeachwa Kwenye Mataa-Washirika Band**

Ni utunzi wake Eddy Sheggy, mwishoni mwa miaka ya 1980, alitunga kibao hiki, cha jamaa aliyedanganywa na mpenzi wake akienda kumsindikiza mjomba wake Uwanja wa Ndege anasafiri, akaenda naye. Kufika huko, kumbe ni mpenzi wake na tiketi amekatiwa. Yeye akaachwa hapo, mpenzi wake na jamaa wakaingia ndani ya ndege.



**Farida-Tabora Jazz Band**

Wimbo huu ulifyatulia kwenye miaka ya 1970 na bendi ya Tabora Jazz Band. Kisa hiki ni cha jamaa aliyemchukua Farida Mwanza na kumleta mjini Dar. Alipokwenda safarini Tanga, aliporudi hakumkuta mwanamke huyo. Alimtoroka na kila kitu kamchukulia. Hapa mwanaume kapigwa.



# Peruzzi kutoa singo mpya

MWIMBAJI na mtunzi wa muziki wa Afriobeats kutoka Nigeria, Peruzzi anatazamia kuwashtua mashabiki wake kwa kutoa singo mpya akishirikiana na mwanamuziki maarufu Olamide Baddo.

Peruzzi, ametumia ukurasa wake wa Instagram kutambulisha kipande cha wimbo huo unaoitwa 'Jah Love Never Fail Me Yet' ambao umenogeshwa vizuri na Olamide.

Wimbo huo ambao una ladha ya Dancehall na Afrobeats, umeegemea zaidi muziki wa Injili, huku Peruzzi mwenyewe akikiri kupata neema ya Mungu.



## Kizz kumbe kapata jiko

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, Oluwatobiloba Daniel Anidugbe, maarufu Kizz Daniel, amethibitisha rasmi kwamba anaishi katika maisha ya ndoa.

Kizz Daniel ametoboa siri hiyo wakati wa mazungumzo yake na mashabiki wake kwenye mtandao wa X wiki hii.

Amesema ni kweli kwa sasa yuko katika maisha ya ndoa baada ya kumwoa mwanamke mwenye mchanganyiko wa makabila ya Igbo na Warr.

Ameeleza kwamba ana furaha kutokana na mke wake kumfunza mambo mengi ambayo huko nyuma alikuwa hayajui.


## Afolayan anogewa kizamani

MWONGOZAJI wa filamu za Nollywood, Kunle Afolayan, amesema ataendelea kutengeneza kazi zinazolenga maisha ya utawala wa zamani wa himaya ya Oyo.

Afolayan tayari amepata mafanikio na filamu yake ya Aníkúlápó, ambayo chini ya wiki mbili ilikuwa imetazamwa kwa saa 8,730,000, kulingana na data ya mtandao wa Netflix.

"Nililazimika kufanya filamu hii ambayo inaelezea maisha ya Saro (Kunle Remi) na Arolake (Bimbo Ademoye) na kugusia kila kitu kuanzia jinsia, ujio wa Uislamu, hadi fitina za Dola ya Oyo ya Kale," amesema.





## 2Baba aachana na meneja wake

SASA ni rasmi kuwa mwanamuziki maarufu nchini Nigeria, 2Baba ameachana na meneja wake Efe Omorogbe baada ya miaka 20 wakiwa wanafanyakazi pamoja.

Habari hizo zilishirikishwa na mtandao wa kijamii wa Now Muzik, ambao unamilikiwa na kampuni ya Efe Omorogbe.

Katika chapisho hilo, Efe Omorogbe, Mkurugenzi wa Sasa Muzik, alitoa shukrani kwa safari yao akieleza kwamba 2Baba kama mmoja wa wanamuziki wakubwa wa Nigeria wa wakati wote.

## Chris Brown amteka Ayra

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, Ayra Starr amekuwa mwanamuziki pekee atakayeambatana na mkali wa R&B wa Marekani, Chris Brown, katika ziara yake ndefu ya kimuziki.

Mwimbaji huyo aliyeteuliwa katika tuzo za Grammy, anatarajiwa kuwa na Brown kama mgeni maalum katika ziara yake inayofahamika kama "11:11" itakayofanyika katika majimbo mbalimbali ya Marekani.

Ayra Starr ataungana na Brown kwa kutumbuiza katika miji 26 ya nchini Marekani na Canada.





## Wengi wahamasika kuhama Ngorongoro

**Novatus Makunga,** NGORONGORO

WANANCHI wanaoishi katika vijiji vilivyoko ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) wameendelea kuhamasika kuhama kwa hiari kwenda nje ya hifadhi hasa katika Kijiji cha Msomera kilichoko Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.

Tayari serikali imewajengea wananchi hao wanaohama kwa hiari miundombinu ya kisasa kama shule, maji, barabara, zahanati, umeme, mawasiliano, huduma za posta, majosho, malisho na mashamba ya kilimo katika kijiji cha Msomera.

Wananchi hao ambao pia wamepewa uhuru wa kuchagua wenyewe maeneo mengine wanahama kwa lengo la kupisha shughuli za uhifadhi.

Jumla ya vijiji 25 viko ndani ya eneo la NCAA vikiwa na wenyeji wa makabila makubwa ya Wamasai ambao kwa asili ni wafugaji, Wadatoga ambao ni wahunzi pamoja na Wahadzabe ambao kwa asili ni wawindaji, waokota matunda na wala mizizi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kapenjiro, Kata ya Naiyobi wilayani Ngorongoro, Mejisho Mollel, alisema hadi sasa katika kijiji chake zaidi ya kaya 235 zimeshajiandikisha kuhama katika kijiji hicho.

Aidha, Diwani wa Naiyobi, Ngeresa Reteti, alisema kwa sasa serikali imeweka utaratibu mzuri wa wananchi kujiandikisha kwenye ofisi za vijiji.

Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Richard Kiiza, alibainisha kuwa kwa sasa serikali imeboresha utaratibu kwa kuwafuata sehemu walipo na zoezi la kuwaandikisha linapokamilika malipo huandaliwa haraka na ndani ya siku zisizozidi 10.

"Tunahakikisha kuwa mwananchi akijiandikisha na kuthaminishiwa mali zake, ndani ya siku kumi taratibu zote ikiwapo malipo zinakamilishwa ili mwananchi ahamishe bila kuchelewa," alisema.

Aidha, Kamishna Kiiza alisema wameongeza timu ya wataalamu kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru mkoani Arusha ili kuwafikia kwa haraka wananchi wanaotaka kujiandikisha bila kuwachelewesha.

# Wanawake wapewa mbinu utafutaji haki

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI wa Shirika la Maendeleo la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, amesema wanawake kwa sasa hawapaswi kusherehekea na kuimba majukwaani kwamba wamefanikiwa.

Badala yake, wanachotakiwa kukifanya ni kukaa na kutafakari mustakabali wa maisha yao katika maendeleo ya familia, taifa na haki zao za msingi watazipataje.

Alikuwa akizungumza jana wakati wa mjadala wa pamoja ulioitishwa na shirika hilo, kujadili kaulimbiu ya Siku ya Wanawake Duniani ya mwaka 2024 na nafasi ya mwanamke katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji utakaofanyika mwaka huu.

Mdahalo huo uliwashirikisha wananchi wa kawaida kutoka wilaya za Moshi, Siha (Kilimanjaro) na Wilaya ya Arumeru (Arusha).

"Tukiangalia kwa ujumla mwaka huu, kauli mbiu iliyotoka ya kutuongoza wanawake inasema wekeza kwa mwanamke kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii.

"Tafsiri yake ni nini? Ni kwamba kunaonekana kuna upungufu mahali. Mtu anapokwambia wekeza kwa mwanamke ni kuendeleza maendeleo ya jamii na ustawi wake. Maana yake tayari kumeonekana kuna upungufu wa uwekezaji.

"Na upungufu huo ndio haya tunayosema yanatokana na mifumo, taratibu, mitizamo iliyojengeka ndani ya jamii na imani, zimeona kwamba huyu labda hawezi kufanya hiki na haruhusiwi kufanya hiki," alisema.

Kutokana na kasoro hizo, alisema matokeo yake wanawake wamejikuta wako hatua kadhaa nyuma na wanaume wako hatua kadhaa mbele yao.

Aidha, alisema jambo moja ambalo ni la kimfumo, wanawake wasipoliwekea nguvu ya pamoja na kujadiliana, na wakatoka na mapendekezo hawataweza kufikia usawa na ustawi tunaoutaka jamii na maisha yao.

"Keki imewekwa mezani wanaokata ni wengine, wewe ulioko jikoni unategemea uletewe kipande cha namna gani? Utaletewa makombo au watakusahau kabisa. Ni lazima tuangalie ni ipi nafasi ya mwanamke katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, ambao tunatarajia kuufanya mwezi Oktoba mwaka huu," alisema.

"Ni lazima mwanamke atambue nafasi yake ina nguvu sana ya kugusa mfumo uliowavuta nyuma, uliowaweka mateka kwa kipindi cha zaidi ya miaka na karne katika maisha yetu," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Rutazaa, TUSONGE inataka kuweka nguvu ya kuangalia uchaguzi wa serikali za mitaa kwenye maeneo ya kuchaguliwa na siyo ya kupendekezwa.

Tujanael Msuya, Mkazi wa Bomambuzi, alisema wanaona kwa sasa ni muhimu wanawake kuingia moja kwa moja kwenye mchakato wa nafasi za kupigiwa kura na wananchi wote.



Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Richard Kiiza akizungumza na wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyopo ndani ya hifadhi hiyo, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# DC aagiza msako walioharibu mifugo

**Na Allan Isack,** HANANG'

MKUU wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara, Janeth Mayanja, ameagiza Jeshi la Polisi wilayani hapa kuwakamata watu wote waliohusika na uhalifu wa kukatakata mifugo kwa mapanga katika kijiji cha Gehandu.

Watu hao wanadaiwa kutenda uhalifu huo kwa kuwa wamekatakata mifugo hiyo kwa mapanga kwa madai kuwa inaharibu msitu wa Gehandu.

"Naagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata watu ambao wametenda uhalifu huu wa kuikata mifugo kwa mapanga ili kukomesha hali hii kutokujirudia tena," alisema Mayanja.

Alisema kutokana na tukio hilo kutokea, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, walipiga yowe kwa kuwa mifugo yao ilikatwakatwa kwa mapanga hivyo kuzua taharuki katika eneo hilo.

Pia aliagiza jeshi hilo kuwakamata wahusika waliojeruhi mifugo na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria haraka iwezekanavyo ili sheria ichukue mkondo wake. Hata hivyo, alitoa rai kwa wananchi kutokujichukulia sheria mkononi kwa kuwa wanapaswa kutoa taarifa kwenye vyombo husika pamoja na kutunza misitu kwa kuwa misitu ni uhai.

"Pamoja na hayo, msitumie hoja ya ukabila na udini kujipenyeza kwenda kuharibu msitu wa Gehandu kwa kuwa unatarajia kunufaisha kizazi cha leo na cha kesho," alisema Mayanja.

Mmoja kati ya wafugaji waliopata hasara ya ng'ombe zake kukatwakatwa, John Nade, ameiomba Serikali kuwachukulia hatua waliohusika na tukio la kukatakata mifugo yao.

"Siyo vyema kuchukua sheria mkononi kwa watu kukatakata mifugo ya wengine bila kuchukuliwa hatua, hivyo tunaiomba serikali ibebe hilo ili lisijirudie tena," alisema. Mfugaji mwingine, Emmanuel Hams, alimshukuru mkuu huyo wa wilaya kwa kuchukua hatua kwa ajili ya kukomesha matukio kama hayo yasiweze kujirudia tena.

Pia Hams alisema hata wao wangeweza kuchukua hatua kwa kulipiza kisasi lakini waliamua kuacha ili sheria ichukue mkondo wake.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, James Qari, alisema watu hao, walikatakata mifugo hiyo, baada ya kuona inachungiwa kwenye msitu wa Gehandu.

Alisema baada ya watu hao kuonywa kutoingiza ng'ombe na mbuzi kwenye msitu huo walichukua sheria mkononi kwa kuikatakata kwa mapanga.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Mwinyi alivyomaliza enzi za kuchoma nywele, kanta, saluni za mwembeni



Picha hii inaonyesha hali halisi ya vinyozi wa zamani waliokuwa wakifanyia kazi chini ya miti enzi hizo.

**Na Adam Fungamwango**

AMEZUNGUMZWA kwa mengi, kisiasa, kijamii na kiuchumi, lakini kuna eneo ambalo limeachwa kusemwa juu ya kipindi cha utawala wa Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi aliyefariki dunia Februari 29, mwaka huu kwenye Hospitali ya Mzena, Kijitonyama, Dar es Salaam na kuzikwa katika Kijiji cha Mangapwani kilichopo Mkoani Kaskazini Unguja, Wilaya ya Kaskazini B.

Mwinyi aliyekuwa Rais wa Tanzania kuanzia mwaka 1985 mpaka 1995, ndiye baba wa mageuzi ya uchumi ya teknolojia nchini, kwani alipoingia alifungua milango ya wawekezaji, bidhaa kutoka nje, pamoja na teknolojia kama televisheni na simu za mkononi ambapo wakati huo havikuwepo nchini.

Naam! Kwetu sisi tuliobahatika kuiona dunia tarehe zile, tuna mengi laivu, aliyotenda mzee huyu. Amefanya mengi, wallah nakwambia! Lakini leo najikita kwenye urembo na vitu vinavyofanana na hivyo.

Katikati ya miaka ya 1970, hadi mwanzoni mwa 1980, kulikuwa na ujio wa baadhi ya wanamuziki nchini kutoka mataifa mbalimbali, ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Afrika Kusini, hasa wa kike, pamoja na majarida mbalimbali yaliyokuwa yakiwaonyesha wanawake mastaa jinsi walivyokuwa wakijipamba na kutengeneza nywele zao.

Ikawapendeza baadhi ya wanawake hasa wake waliokuwa wa kisasa enzi hizo. Tatizo lilikuwa ni teknolojia duni.

Kilichotumika hapo ni kuchoma kuchukua kitu chochote chenye asili ya bati na kukiweka motoni.

Baada ya hapo kinapitishwa kwenye nywele ili kuzifanywa ziwe laini na zinyooke na kuwa ndefu.

Baadaye wengine wakawa wanapitisha pasi ya mkaa, na baadaye kidogo ikaja kukawa maendeleo kwani kulikuwa na chanuo za chuma, ambazo zote kazi ilikuwa ni hiyo hiyo ya kutengeneza nywele za kinamama ili ziwe kama zimewekwa 'relaxer.'

Kazi hiyo ilifanywa kwa uangalifu mkubwa na aliyekuwa anachoma nywele za mwenzake ili asimuunguze.

Ukiachilia mbali madada wa mjini, au wa kisasa enzi hizo, huku uswahilini zikikaribia nyakati za sikukuu, iwe Krismasi, Pasaka, au Idd El Fitri, utaona jinsi wasichana wanavyohangaika ili wapendeze.

Kazi inakuwa ni hiyo hiyo, kuchukua vibati, pasi za mkaa na wale kwenye chanuo za chuma sawa.

Vitawekwa kwenye moto, na kupitishwa kwenye nywele kwa ajili ya kupata urembo wanaouhitaji.

Baada ya hapo kuna vidonge vyeusi ambavyo vinaloweshwa kwenye maji na kupakwa kichwani ili nywele zizidi kuwa nyeusi na kuvutia, wengine wanaweka dawa aina ya kanta, na wale wenzangu na mimi wa uswazi wao wanaweza kuchoma hata mpira wa manati, ili mradi tu kupata weusi wa kupaka kwenye nywele zilizochomwa.

Tatizo ni kwamba sikukuu ikipita na kukaa sana zinakuwa kama 'zimelambwa na mbwa', inabidi zikatwe, au zifanyiwe utaratibu mwingine wa kuchomwa tena. Haya ndiyo yalikuwa maisha ya urembo enzi hizo kwa kinadada na kinamama.

Ukitoka kwa kinadada na kina mama, tunakwenda kwa kinababa, vijana mpaka watoto.

Nywele zao walikuwa wakinyoa kwa vinyozi waliokuwa wanafanya kazi hizo chini ya miti mikubwa kama miembe, mikorosho na mingine inayofanana na hiyo.

Kwa wale waliokuwa watoto wanakumbuka, siku chache kabla ya kufungua shule, au sikukuu zile nilizozitaja mwanzo, wanapelekwa na wazazi wake kwa vinyozi wa mwembeni na kunyolewa kwa kutumia mkasi na wembe.

Watu wazima nao walikuwa wanatumia saluni hizo za chini ya miembe kwenda kushevu ndevu na kurekebisha nywele zao.

Mbali na kivuli wenye upepo mwanana, vinyozi hao walikuwa wanaegemeza vioo vyao kwenye mwembe kama ambavyo picha inaonekana.

Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya wakati huo, kabla ya kuingia Rais Mwinyi, ambaye alifungua milango ya mambo mbalimbali, uchumi, uwekezaji, makampuni binafsi na bidhaa mbalimbali kuagizwa kutoka nje na kuingia nchini bila masharti mengi na magumu.

Hapo ndipo vifaa vya kisasa vya urembo viliingia na mambo ya kuchoma nywele kwa namna ya hatari ilikoma, pamoja na kunyoa nywele chini ya miti.

Ni kwamba tuliona sasa wanawake wakiweka dawa za kisasa, wakipiga 'curly kitty' na 'relaxer.'

Awali kinamama walikuwa wakipambana tu majumbani, lakini baadaye ikafungua fursa kwa wale wanaojua, kufungua maeneo ya huduma hizo na kuziita saluni za kike.

Vinyozi nao wakaachana na kunyoa chini ya miembe, nao wakatengeneza maeneo ya kisasa wakaziita saluni za kiume.

Cha ajabu ni kwamba vinyozi wa zamani chini ya miembe wengi walikuwa watu wazima, lakini kwa sasa wanyoa saluni za kisasa ni vijana tu wadogo.

**Tuma meseji 0716 350534**



Hivi ndivyo wanawake wa zamani walivyokuwa wakitaka nywele zao ziwe kabla ya kuingia saluni za kike na vifaa vyake nchini, wakawa wanazichoma kwa bati, pasi ya mkaa na chanuo la chuma baada ya kuwekwa kwenye moto.

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani kujenga bandari Gaza

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, anatarajiwa kutangaza kwamba jeshi la nchi yake litajenga bandari katika eneo la Ukanda wa Gaza.

Maofisa wakuu wa serikali walisema ujenzi huo wa bandari utatekelezwa ili kusaidia kuingiza misaada ya kibinadamu katika eneo hilo.

Bandari hiyo ya muda itaongeza kiwango cha misaada ya kibinadamu kwa Wapalestina kwa kuingiza shehena kubwa kwa kila siku.

Hata hivyo, bandari hiyo haitajumuisha wanajeshi wa ardhini wa nchi hiyo watakaoingia Gaza.

Umoja wa Mataifa umeonya kuwa robo ya watu wa Palestina wanakabiliwa na njaa.

Bandari hiyo itachukua wiki kadhaa kuanzishwa kujengwa kwake na itaweza kupokea meli kubwa zinazobeba chakula, dawa za maji na makazi ya muda.

Usafirishaji wa awali wa vifaa vya ujenzi utawasili kupitia Cyprus, ambapo ukaguzi wa usalama wa Israel utafanyika.

Rais Biden anatarajiwa kutoa tangazo hilo wakati wa hotuba jana jioni.

Jeshi la Israel lilianzisha mashambulizi ya anga na ardhini katika Ukanda wa Gaza baada ya Oktoba 7, mwaka jana wanamgambo wa Hamas kuingia ndani ya Israel na kushambulia watu.

Jumla ya watu 1,200 waliuawa na wengine 253 walichukuliwa mateka.

Katika mapigano hayo, Wapalestina 30,800 wameuawa kulingana na wizara ya afya ya eneo hilo inayosimamiwa na Hamas.

**BBC**

# Waasi M23 wauteka mji muhimu

**GOMA,** DRC

WAASI wa kundi la M23 wamelichukua eneo jingine baada ya mapambano makali ya siku tatu na jeshi la serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Mpaka jana waasi wa M23 waliuteka mji wa Kibirizi na kusababisha maelfu ya watu kuyakimbia makazi yao kwenda kutafuta hifadhi maeneo mengine.

Kundi hilo lilikuwa likiudhibiti mji huo ulioko kilometa 30 upande wa Kaskazini Mashariki mwa mji wa Goma.

Ofisa mmoja wa utawala katika eneo hilo alilielezea shirika la habari la AFP kwamba, M23 waliuteka mji huo baada ya kufyatuliana risasi na wanajeshi wa DRC na wapiganaji wanaoiunga mkono serikali.

Mkazi mwingine Gervais Kambale, kutoka eneo la karibu la Kanyayonga ambako raia wengi wamekimbilia kwa wiki nzima, alisema wameshuhudia mamia ya watu wakiwa njiani wakikimbia mapigano.

Kambale alieleza kwamba baadhi ya watu wanalala njiani na hakuna shirika la kibinadamu linalowawahudumia kwa sasa.

Umoja wa Mataifa ulisema zaidi ya watu 100,000 wamekosa makazi ndani ya wiki hii, wengi ni kutoka mji wa Nyanzale ulioko mkoa wa Kivu Kaskazini.

Ofisa mmoja wa wapiganaji walio upande wa serikali alithibitisha taarifa hizo akisema kuwa adui yuko Kibirizi na bado wanapigana kuhakikisha wanaukomboa.

Kundi la waasi wa M23 lilianzisha mashambulizi mnamo Jumatatu dhidi ya mji kadhaa, kilometa 70 kutoka mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini wa Goma na kupanua udhibiti wake kuelekea upande wa Kaskazini katika maeneo ya Rutshuru na Masisi.

Mapigano mengine yaliripotiwa kwenye mji wa Sake ulioko kilometa 20 magharibi mwa Goma.

Takribani raia 15 ikiwamo watoto wameuawa katika eneo la Nyanzale katika mashambulizi ya mabomu dhidi ya maeneo wanayoishi kuanzia Jumatatu.

Baada ya waasi hao kutoweka katika kipindi cha miaka minane, waliibuka tena upya na kuanzisha mashambulizi mwishoni mwa 2021.

Walidhibiti maeneo mengi ya Kivu kaskazini na kukata mawasiliano na mji mkuu wake wa Goma.

Kulingana ripoti ya DRC, Umoja wa Mataifa na mataifa ya magharibi, nchi jirani ya Rwanda inahusika kuunga mkono M23, lakini nchi hiyo inakana.

Umoja wa Mataifa unakadiria kwamba hadi kufikia mwisho wa 2023, watu wapatao milioni 7 walikosa makazi nchini DRC wakiwamo milioni 2.5 katika eneo la Kivu Kaskazini pekee.

Wakati huo huo, serikali ya DRC imekanusha ripoti kwamba imetia saini mkataba wa ushirikiano wa kijeshi na nchi ya Russia.

"Hadi sasa, hakuna makubaliano ya ushirikiano wa kijeshi yaliyotiwa saini hivi karibuni kati ya Russia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo," ilisema wizara ya mawasiliano na vyombo vya habari ya nchi hiyo.

Taarifa hiyo inafuatia makala iliyochapishwa na shirika la habari la serikali ya Russia (TASS) iliyotoka Jumanne, ikieleza serikali ya nchi hiyo iliidhinisha rasimu ya makubaliano ya ushirikiano wa kijeshi na DRC.

TASS, ikitoa mfano wa hati ya serikali, iliripoti kwamba makubaliano hayo yalihusisha mazoezi ya pamoja, mafunzo ya kijeshi na ziara za meli na ndege za kivita kwa mwaliko au ombi maalumu.

Serikali ya DRC ilisema rasimu hiyo ya makubaliano ilianzishwa na nchi hizo mbili mwaka 1999, lakini bado haijatiwa saini.

**DW**



Raia wakiwa njiani kuukimbia mji wa Kibirizi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya waasi wa M23 kuuteka na kuudhibiti juzi. **PICHA: AP**

# Guterres ataka kusitishwa mapigano Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ametoa wito wa kusitishwa haraka mapigano yanayoendelea nchini Sudan.

Mapigano kati ya jeshi la serikali na wapiganaji wa kikosi cha dharura cha kijeshi (RSF) yamedumu kwa mwaka mmoja na kusababisha maafa kwa raia.

Guterres alizitaka pande mbili zinazozozana kusitisha mapigano wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani ambao unaanza wiki inayokuja.

Wito huo unakuja wakati wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wanajadili rasimu ya azimio la Uingereza linalotaka kusitishwa mara moja kwa mapigano na kuruhusu utoaji wa misaada ya kibinadamu.

Rasimu hiyo ilitarajiwa kupigiwa kura jana.

Alisema kusitishwa kwa uhasama lazima kutasababisha kunyamaza kabisa kwa bunduki na kuweka njia thabiti kuelekea amani ya kudumu.

Guterres alionya kwamba mzozo huo umefikia kiwango cha juu na kwamba hali ya haki za binadamu inaendelea kudorora.

Mapigano hayo yanahatarisha kuzusha tatizo kubwa la njaa duniani, huku kukiwa na ripoti za watoto wanaokufa kutokana na utapiamlo.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**FLORENTINA NYAMWIZA MUTAFUNGWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S233/0013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. MARY'S MAZINDE JUU** mwaka 1997. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/31151/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HERIETH K. AUGUSTINE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S0249-0028** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LORETO GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007, Cheti hiki kimepotea mkoani Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/RB/5246/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA.



**FIDELIS PETER KIMANGO** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE522883** iliyotolewa uhamiaji makao makuu DAR ES SALAAM PCO. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/30458/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MUSTAKIM ASHIRAFU LIKUA** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye index namba **PS020246/136** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia DIAMOND PRIMARY SCHOOL mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/13229/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHEDY JUMA SEIF** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T544 BTK** YENYE CHESISI NAMBA: **VZJ950006714** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **IRI/IRI/RB/170546/2023.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**CRIMINAL/MISC/CIVIL ,APPEAL, CASE/MATR, CAUSE/REV, PROB ADM**

**CAUSE NO.2341/2024**

**MMT HARDWARE.......................................INTIFF/APPELLANT**
**OSWARD SHEDRACK MKALAWA AND**
**VENANCE THEOPHIL MSOFFE...... ANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention/Hearing on 02 day of 04, 2024 at 9.00am
Before Hon T.KANIKI..............................PRM/SRM
YOUR ARE require to appear in this Court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.
Given under my hand and the seal of the Court this 08/03/day of 2024.

DISRTRICT RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 8 YA 2024**

**KUDRA SHABANI MKUYA..........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **SALEHE RICHARD MLIMBO**
2. **JULIUS CHRISTINA NYAMBO**
3. **BI SAIDAT KITINDE..............................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

1. **SALEHE RICHARD MLIMBO**
2. **JULIUS CHRISTINA NYAMBO**
3. **BI SAIDAT KITINDE**

Popote mlipo mnataarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 21/3/2024 mbele ya Mwenyekiti M.KHASIM ninyi wenyewe au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 29 mwezi February, 2024.

M.KHASIM
MWENYEKITI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha MJINI ( IJC) Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na. 54/2024**

**JINA LA MDAI ........... SAMWEL MWITA**

**JINA LA MDAIWA .................... ALEX GUZEYE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA**
**ALEX GUZEYE**
**MOROGORO**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH. 6,003,700/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 12 mwezi 03 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 06 Mwezi 03 Mwaka 2024.

HAKIMU
PRINCIPAL
PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 14 YA MWAKA 2024**

**BAINA YA**

**NEEMA WELLU ........................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**RAHELI MMARI ...................................... MDAIWA**

**KWA:**
**RAHELI MMARI**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 13.03.2024 saa 3:00 asubuhi. Kajili ya kutaja.
ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07 ya mwezi Machi, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,

---

**IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3734 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late JOYCE GIDION NYAU of Dodoma within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**SAME ELIEZA MAWELE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 03 Day of 04, 2024

Dated at Dodoma this 07 Day of 03, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MAHAKAMA)**

**KATIKA MAHALAMA YA MWANZO ENABOISHU WILAYA YA ARUMERU**

**SHAURI LA MADAI NA.3 YA 2023**

**ZAKAYO MEVALARI..........................................MDAI**

**DHIDI YA**

**LOSERIAN SANINGO.....................................MDAIWA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS GENERAL)**
**(MCA NA.2/1984)**

**Kwa Loserian Saningo**
**Olorieni**

Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka/madai kuwa shahidi kama ifuatavyo
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
**UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe 21/3/2024 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili ushauri hili liweze kusikilizwa.
USIKOSE KUHUDHURIA
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/F Na. 114 A Sura 16K/A. Hivyo mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria.
**HATI HII IMETOLEWA NA [illegible] YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 7/3/[illegible]**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO ENABOISHU

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**KATIKA MASIJALA NDOGO YA GEITA**

**KESI YA RUFAA NO 2885 YA MWAKA 2024**

**DISMAS KANYEMELA .........................MKATA RUFAA**

**DHIDI YA**

**KAROLIUS MISUNGWI (Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu COSTANTINE MISUNGWI) & 6 OTHERS......WAJIBU RUFAA**

**Kwa:**
**Magreth Costantine Misungwi**
**Popote Ulipo**

**KUITWA SHAURINI**

Shauri tajwa limefunguliwa dhidi yenu hapa mahakamani na kupangiwa kusikilizwa tarehe 13/3/2024 mbele ya Mh.K.Mhina Jaji saa tatu kamili asubuhi.
Unatakiwa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako bila kukosa
Unatahadharishwa kuwa endapo hautafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu pamoja na Chapa ya mahakama hii leo tarehe 22/2/2024

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU GEITA

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichofananishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-3

**Na Adam Fungamwangwo (0716 350534)**




Alichodhani kuwa yeyote ambaye alikuwa amekaa siti ya dirishani, kama ni mwanaume, atakapofika na kumtazama tu, basi asingeweza kufanya kitu chochote. Angemkubalia kukaa dirishani bila masharti yoyote. Leo haikuwa hivyo.

"Ni mwanaume wa wapi huyu?" Mariamu akajiuliza.

"Dada nadhani umesikia nilichokuambia." Akarudia tena Kamal kwa sauti ya upole na unyeyekevu, japo alichokuwa akikitaka hakikuwa cha unyenyekevu.

Mariamu sasa akaamua tu kukubali yaishe. "Nakupisha kaka yangu." Akasema kwa sauti ya hasira kidogo iliyochanganyikana na aibu. Kwa mara ya kwanza ndipo alipogundua kuwa si kwa asilimia zote uzuri au urembo alionao unaweza kumpa au kumsaidia kila kitu. Akakumbuka usia wa marehemu mama yake aliowahi kumwambia.

"Mwanangu usibabaishwe na uzuri ulionao. Usitumie uzuri wako kutaka kukurahisishia mambo yako. Akili, juhudi na maarifa uliyonayo ndiyo ikupatie namna ya kuishi, siyo uzuri.

Wanaume wanaokufuafuata hawakufuati wewe, wanafuata kuufyonza uzuri na urembo ulionao, ili baadaye ukiisha wakuache kama makapi ya kipande cha muwa. Kila unachotaka kufanya, kununua, fanya kwa juhudi zako, siyo kupewa au kusaidiwa na wanaume. Hawana msaada wa kweli. Kuna kitu watakuwa wahahitaji." Mariamu alikumbuka maneno ya marehemu mama yake akiwa anasimama, na kupishana na Kamal.

Sakata likaisha kwa Kamal kuwa mshindi akiwa amejikatia zake upande wa dirishani, Mariamu akiwa katika siti hiyo hiyo upande mwingine.

Tayari basi lilishaanza kutafuna lami kuisaka Dar es Salaam. Kamal na Mariamu walikuwa wamekaa siti moja, lakini mmoja upande wa dirishani.

Pamoja na kwamba si lazima abiria wanaokaa siti moja kuongea, lakini kutokana na kilichotokea, walikuwa wamenuniana.

Kamal anaangalia dirishani, Mariamu mbele, lakini mara moja moja, macho ya kila mmoja kuna wakati yanaiba kumtazama mwenzake.

"Janaume lina roho mbaya hili.! Sijui kabila gani hili." Alijisemea moyoni huku akimuibia jicho baada ya kichwa cha Kamal kugeukia kutazama dirishani.

Kamal naye akiona msichana anaangalia kitu kwenye pochi yake, au amezubaa, anaiba jicho na kumtazama kwa chati.

"Msichana mzuri huyu! Sijui ametokea wapi?" Alijiuliza mwenyewe. Hata hivyo tayari alikuwa amemuudhi. Hilo hakujutia sana, alichofurahi kuuonyesha umma wa abiria kuwa yeye si dhaifu kwa mwanamke.

Wao walidhani akija na kumkuta mrembo kama yule ataufyata mkia, atakaa tu na hatomuuliza lolote ili wamcheke au wapate la kuongea, lakini kwa makusudi amewaonyesha yeye si kama wanaume wanaowafikiria au kama wao.

Mwendo wa basi hilo ulianza kuwakera baadhi ya abiria. Haukuwa wa kuvutia. Mmoja akashindwa kujizuia.

"Dereva eee, unaendeshaje kama unapeleka harusi bwana, watu tunataka kufika Dar mapema ujue."

Dereva hakujibu lolote, aliendelea kuendesha basi kwa mwendo wa taratibu huku wale waliokuwa wakitaka mwendo wa kasi wakiongea maneno yao yote ya kejeli na dharau kwa dereva.

Lilipofika Bwawani, kilometa 49 kutoka Morogoro mjini. Kwa kawaida hutumika dakika 36, lakini dereva alitumia dakika 50, lilisimama.

Hakukuwa na maelezo yoyote, lakini kila mmoja alitambua. Kama hujui kusoma hata picha nayo huioni? Lilikuwa limeharibika.

"Samahani ndugu abiria, basi letu limeharibika kidogo, tumepiga simu Morogoro mjini kuna kifaa kinaletwa ili kukifunga tu safari yetu iweze kuendelea." Ilikuwa ni sauti ya kondakta wa basi hilo.

**"Samahani ndugu abiria, basi letu limeharibika kidogo, tumepiga simu Morogoro mjini kuna kifaa kinaletwa ili kukifunga tu safari yetu iweze kuendelea." Ilikuwa ni sauti ya kondakta wa basi hilo.**

Abiria wengine walielewa, wengine wakalaumu na wapo ambao hawakusema lolote.

Ni wachache tu waliobaki ndani ya basi. Wengi waliteremka. Tayari ilikuwa saa 11:00 jioni, bado kweupe.

Haikuwa kituoni kabisa, ilikuwa ni nyuma kidogo. Abiria waliteremka na kuanza kuzagaa huku na huko. Wengine walikwenda kukaa kwenye majani na kuanza kupiga stori. Wengine waliamua kuingia kwenye mitaa ya maeneo hayo.

Siku zote wanywa pombe na wavuta sigara huwa hawana ugeni sehemu yoyote ile. Wakifika sehemu utakuta haraka wameshapata wenyeji wao wanaokwenda kuwaonyesha maeneo yao ya kujidai. Hivi ndivyo ilivyokuwa. Walikisia basi haliwezi kutoka hapo chini ya saa moja nzima.

Mariamu alikwenda mbali kidogo na kukaa kwenye safu ya majani mabichi ambayo yalikuwa yametanda kama ya uwanja kwenye uwanja wa mpira.

Wakati wengine wamekaa makundi makundi yeye alikaa peke yake. Kwa kilichotokea mle ndani ya basi, hakuna hata mwanaume mmoja aliyekwenda kumsogelea na kumsemesha chochote. Kila mmoja aliogopa majibu atakayojibiwa. Ogopa majibu ya mwanamke aliyekasirika. Alionekana kuwa bize tu na simu yake ya 'tachi.' Hakuwa na taimu ya mtu.

Kamal alijiingiza kwenye mitaa ya vijijini, lakini hakuwa mnywaji wala mvuta sigara, hivyo dakika 10 zilimtosha huko na akarejea tena eneo la barabara ya Morogoro kusubiri matengenezo ya basi.

Katika angalia yake, akamuona msichana aliyekaa naye siti moja amekaa peke yake kwenye nyasi akili yake yote ikionekana kwenye simu yake.

Akaamua kusogea kwa hatua za taratibu kuelekea alipo. Mariamu hakutambua kama kuna mtu anamfuata.

Alipofika karibu yake, akiwa nyuma ya mgongo wa anayemfuata alisimama. Alibakisha kama hatua tatu za mtu mzima kufikia.

"Vipi, mrembo, mbona umekaa huku peke yako?"

Sauti hiyo nzito kidogo na yenye utulivu ikionekana haina chembe ya wasiwasi, ilimshtua Mariamu aliyekuwa makini kuangalia vikatuni kwenye simu yake ya mkononi.

Macho yake yalikutana na mtu yule yule aliyemkwaza ndani ya basi. Akakunja sura kwa namna ya kuonyesha hakupendezwa kwa mgeni yule kufika pale.

Akamwangalia kuanzia chini na kumpandisha hadi juu. Halafu akafyonya.

**Itaendelea Jumamosi**

HABARI MICHEZO

# NGAWINA ATAKA USHIRIKIANO SINGIDA FG, AWATAJA SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA wa muda wa Singida Fountain Gate FC, Ngawina Ngawina, amewaomba wachezaji wa timu hiyo kumpa ushirikiano ili kupunguza presha iliyopo baada ya kutokuwa na matokeo mazuri katika michezo mitatu mfululizo iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Singida Fountain Gate FC walipoteza mbili dhidi ya Mtibwa Sugar kwa kuchapwa mabao 2 -0 baadaye ikafungwa goli 1-0 na Azam FC wakiwa nyumbani huku pia walilazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Tabora United.

Akizungumza na Nipashe jana, Ngawina alisema anafurahi kujiunga na benchi la timu hiyo na anaimani ndani ya mikono yake watafanya vizuri katika mchezo ujao dhidi ya Simba.

Ngawina alisema endapo atapata ushirikiano kutoka kwa wachezaji ambao baadhi anawafahamu, uwezo wa kufikia malengo wanao na watamaliza presha iliyopo sasa.

„Kupunguza presha hiyo ni kutulia na kufuata maelekezo ninayowapa katika uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kujiandaa dhidi ya Simba, tutahakikisha tunapambana kucheza katika kiwango bora ili tupate matokeo chanya.

Tunafahamu Simba imetoka kupoteza kwenye Uwanja wa Jamhuri (Morogoro), na tunakutana nao, hawatakuja kama walivyocheza mechi za nyuma, kwa sababu hiyo tunatakiwa kushikamana na kwa upande wa wachezaji kufuata kile ninachowapa na kuhamisha uwanja wa mechi," alisema Ngawina.

Kocha huyo amekabidhiwa majukumu ya kukinoa kikosi cha Singida Fountain Gate FC baada ya uongozi wa timu hiyo kutimua benchi lote la ufundi.

Aliyekuwa kipa wa zamani wa Simba na Yanga, Ally Mustapha 'Barthez' naye ametua katika kikosi hicho kwa mkataba wa muda mfupi mpaka pale itakavyotangazwa vinginevyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Singida FG yenye pointi 21 iko kwenye nafasi ya 11 wakati Mtibwa Sugar yenye maskani yake Turiani, Morogoro inaendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi 12 mkononi na imecheza michezo 18.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mzambarauni (waliovaa bips) wakichuana na wenzao kutoka Shule ya Msingi Gerezani katika mpira wa magongo kwenye viwanja vya JKM Park jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtemi akerwa utimamu Simba

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mtemi Ramadhani, amesema kwa muda mrefu wachezaji wa Simba wamekosa utimamu wa mwili hali ambayo inawafanya wanashindwa kuonyesha kiwango kizuri kama cha watani zao, Yanga.

Mtemi, beki aliyewika mwanzoni mwa miaka ya 1980, akiwa na Timu ya Waziri Mkuu, Dodoma na baadaye Simba akihudumu alisema anatamani aende kwenye kambi ya timu hiyo na kuangalia mazoezi yao ili ajue kama kweli wanafanya mazoezi ya aina hiyo.

„Ukiangalia utimamu wa mwili wa wachezaji wa Simba na Yanga ni vitu viwili tofauti, wenzetu ‚fiziki' sana, unawaona kabisa wakicheza wako timamu kimwili.

Nashangaa sisi kwa nini hatuwi hivyo, unaona kabisa timu inakuwa dhaifu, sisi zamani tulikuwa tunakimbia, tunafanya mazoezi ya kutosha tunakwenda ufukweni, tunakuwa tuko vizuri, lakini kwa miaka ya hivi karibuni ikikutana na timu yoyote ambayo inafanya mazoezi vizuri inakuwa ni mtihani mkubwa," alisema Mtemi ambaye aliwahi kufanya kazi katika Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF).

Mtemi ambaye ni mmoja wa wachezaji waliocheza AFCON ya kwanza nchini Nigeria iliyofanyika mwaka 1980, alisema suala hili huwa linamtatiza sana na anatamani hata kwenda kambini akaongee na makocha na wachezaji kuhusu suala hilo, lakini hata kwenda kuhudhuria mazoezi yao.

„Mimi natamani niingine katika kambi ya Simba niwaambie tatizo ni nini, kwa nini hii timu haiko vizuri katika utimilifu wa mwili," alisema mchezaji huyo wa zamani ambaye mwaka 1984 alifunga bao la pili Uwanja wa CCM Kirumba, Simba ikiifunga Al Ahly mabao 2-1, Kombe la Shirikisho barani Afrika.

## Malindi nje Kombe la ZFF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKONGWE Malindi SC wameondolewa katika hatua ya 32 bora ya mashindano ya Kombe la FA Zanzibar baada ya kufungwa bao 1-0 na Nyangobo inayoshiriki Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi huku Ngome FC nayo imekubali kichapo cha penalti 4-3 kutoka kwa Taifa Jang'ombe.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wamefanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuifunga Sharp Boys kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja bao 1-0 mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Cairo ulioko Kiwengwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Nyangobo FC, Ussi Ali Ussi, alisema haikuwa kazi rahisi kuwaondoa vigogo wa Ligi Kuu Zanzibar, Malindi katika michuano hiyo.

Ussi alisema licha ya kupata bahati ya kusonga mbele lakini wachezaji wake walicheza kwa utulivu mkubwa na umakini na walishuka dimbani wakijua wanacheza na wakongwe wa soka visiwani hapa.

Alisema tangu awali malengo ya timu yake yalikuwa ni kucheza soka la ushindani na kuonyesha uwezo wa juu bila kujali wanakutana na wazoefu.

„Tumefanikiwa tena kusonga mbele katika hatua hii ngumu ambayo tunakutana na vigogo vya Ligi Kuu, hii kwetu ni mafanikio kwa sababu lengo letu ni kuendelea kupata uzoefu na kucheza soka la ushindani bila kujali tunacheza na nani," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, amekiri mchezo wao dhidi ya Sharp Boys ulikuwa mgumu katika dakika zote 90.

Msimu alisema wapinzani wao waliingia na mbinu ya kukamia mchezo jambo liloipa timu yake wakati mgumu na kusababisha washambuliaji wake washindwe kufanya maamuzi pale wanapomiliki mpira.

"Ni kawaida unapokutana na timu hizi za madaraja ya chini mechi inakuwa ngumu sana, mbinu kubwa wanayotumia ni kukukaba na kutumia nguvu kubwa, sasa kama mwalimu unatakiwa uje na mbinu ya kushambulia zaidi pale unapomiliki mpira," Ussi alisema.

Mashindano hayo ya Kombe la FA yataendelea tena leo kwenye Uwanja wa Mau A Mafunzo watawaalika Negro FC kuanzia saa 8:00 mchana na baadaye New City FC watavaana na New King FC huku kwenye Uwanja wa Mau B JKU itakutana na Union Rangers na jioni KVZ itapambana na Mwembe Makumbi City na Raskazone FC watachuana na Black Mamba.

## ZISIKUPITE

### TUCHEL KUREJEA CHELSEA

THOMAS Tuchel amelenga kurejea kuifundisha Chelsea atakapoondoka Bayern Munich majira ya joto, lakini kocha huyo wa Ujerumani pia anavutiwa na Manchester United na Barcelona. ***(Sky Sports)***

### LIVERPOOL YAINGIA SOKONI

WAMILIKI wa Liverpool walikutana na Michael Edwards Jumapili iliyopita katika majaribio yao ya kumshawishi mkurugenzi wa zamani wa michezo wa klabu hiyo kuunda nafasi mpya baada ya Jurgen Klopp kuondoka Anfield**.** ***(Mail)***

### ARSENAL KUSAJILI STRAIKA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema kiwango cha kuvutia cha timu yake mbele ya lango hakitabadilisha mipango ya klabu hiyo ya uhamisho, huku bado wakitarajiwa kusajili mshambuliaji katika majira ya joto. ***(ESPN)***

### ZINCHENKO AGOMBEWA ULAYA

MLINZI wa kushoto wa Arsenal, Oleksandr Zinchenko, analengwa na Newcastle United na Bayern Munich, huku washikabunduki wakitaka euro milioni 38.5 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ukraine mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Transfers)***

### WINGA WA NAPOLI SOKONI

WAKALA wa winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ataondoka Napoli ikiwa klabu hiyo ya Italia itapokea ofa ambayo haiwezi kukataa. ***(Gazzetta dello Sport)***

### UNITED YAMZUIA MASON

MABOSI wa Manchester United wanatarajiwa kumzuia, Mason Greenwood, kwenda Marekani kwa ziara ya kujiandaa na msimu mpya baada ya mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 22 kurejea kutoka Getafe alipokuwa kwa mkopo. ***(Star)***

### CHELSEA YASAKA FAIDA

CHELSEA itategemea mauzo ya faida msimu huu ili kufadhili mipango yao ya uhamisho, huku bodi ya The Blues hao kilenga kuwaondoa wachezaji wa nyumbani akiwamo kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24, beki wake, Trevoh Chalobah (24), na mshambuliaji wa Albania, Armando Broja (22). ***(Team talks)***

### SUMMERVILLE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA imeweka winga kuwa moja ya vipaumbele vyao, huku mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri chini ya miaka 21 wa Leeds United, Crysencio Summerville, akiwa mmoja wa walengwa wao wakuu. ***(Team Talks)***

### MAINOO KUULA UNITED

KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo ya awali kuhusu kuongeza mkataba wa kiungo wa kati wa England, Kobbie Mainoo, kufuatia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kuwa na kiwango kizuri msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

### UGORJI AGEUKA LULU

KLABU za Ligi Kuu England zinamfuatilia mshambuliaji wa Birmingham City aliye na umri wa chini ya miaka 16, Tobey Ugorji. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND AELEZA HISIA KUTWAA MATAJI MATATU

●●●Mshambuliaji huyo amshangaa Trent ambaye hajafikia rekodi...

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Erling Haaland, amejibu madai ya Trent Alexander-Arnold, kuhusu mataji ya Liverpool yana maana zaidi ya City, akisema beki huyo hajui hisia za kushinda mataji matatu.

Mchuano mkali kati ya timu mbili za England zilizofanya vizuri zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita umeibuka mbele ya klabu hizo mbili bora za sasa za Ligi Kuu England ambazo zitamenyana kesho kwenye Uwanja wa Anfield.

“Kama anataka kusema hivyo, sawa. Nimekuwa hapa mwaka mmoja na nikashinda mataji matatu na ilikuwa ni hisia nzuri, sidhani kama anajua vizuri hisia hizi,” alisema Haaland akiiambia Sky Sports.

Ushindi wa Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka jana. „Ndivyo nilivyohisi msimu uliopita na ilikuwa nzuri sana. “Wanaweza kuongea kadri wanavyotaka, au anaweza kuzungumza vile anavyotaka. Sijui kwa nini anafanya hivyo, lakini sijali.”

City wameshinda mataji 14 tangu Pep Guardiola achukue mikoba kama mwaka 2016, ikilinganishwa na mataji saba ya Liverpool tangu Jurgen Klopp atue klabuni hapo.

Katika mahojiano na jarida la Four Four Two, Alexander-Arnold alisema uwezo wa matumizi wa timu hizo mbili unamaanisha mataji ya Liverpool yana thamani zaidi.

“Tukikumbuka enzi hizi, ingawa (City) imeshinda mataji mengi kuliko sisi na pengine imekuwa na mafanikio zaidi, mataji yetu yatakuwa na maana zaidi kwetu na kwa msingi wa mashabiki wetu kwa sababu ya hali za kifedha katika klabu zote mbili,” alisema.

“Jinsi klabu zote mbili zimejenga timu zao na jinsi tulivyofanya, pengine ina maana zaidi kwa mashabiki wetu. Ni ngumu. Tunapingana na mashine ambayo imeundwa kushinda, hiyo ndiyo njia rahisi ya kuielezea City.““

Liverpool wanaongoza dhidi ya Manchester City kwa pointi moja huku zikiwa zimesalia mechi 11 kabla ya mechi yao ya kesho.

# BARCA YAFIKIRIA KUMUUZA PEDRI

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inatajwa inafikiria kumuuza, Pedri baada ya kiungo huyo kupata jeraha lingine wikiendi.

Pedri alipata tatizo la misuli kabla ya kwenda mapumziko Barca wakitoka sare ya bila kufungana na Athletic Club, akionekana kupata jeraha hilo wakati akipiga pasi kwa Raphinha.

Kiungo huyo amegundulika kupata jeraha huku kocha, Xavi Hernandez, akikiri Pedri anaweza kuwa nje ya uwanja "kwa muda mrefu".

Licha ya kuwa na umri wa miaka 21 pekee, Pedri amekosa michezo 69 kutokana na majeraha mbalimbali ya misuli ya paja - hasa kukosa kucheza kwa miezi mitatu msimu huu tayari baada ya kuchechemea wakati wa mazoezi Agosti, mwishoni mwaka jana.

Kutokana na matatizo ya mara kwa mara ya Pedri, AS imeripoti La Blaugrana wanatamani kupata suluhu yake.

Ingawa klabu ingependa kuendelea kumshikilia kiungo huyo mchanga, ripoti inasema suluhu moja ambayo halijazuiwa ni kupunguza hasara na kumuuza Pedri siku zijazo.

Ripoti kutoka Hispania hapo awali zilidokeza Bayern Munich na Paris Saint-Germain zilikuwa zinamwania kiungo huyo, huku Juni, mwaka 2023, AS ikisema kiungo huyo alikuwa na ofa kabambe ya euro milioni 100 iliyokataliwa na Barca.

Barcelona pia wamekuwa wakihusishwa na wachezaji kadhaa wanaotarajiwa kusajiliwa katika safu ya kiungo kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto.

Nyota wa Arsenal, Jorginho anasemekana "kufurahishwa" na nia iliyoonyeshwa na klabu hiyo ya Katalunya.




## Klopp aelezea jeraha la Konate

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema kumtoa Ibrahima Konate katika mchezo wa Ligi ya Europa waliposhinda mabao 5-1 dhidi ya Sparta Prague ilikuwa ni tahadhari tu.

Wekundu hao walipata ushindi wa 16 bora wa mkondo wa kwanza katika mji mkuu wa Czech lakini kulikuwa na hofu kubwa Konate alipotolewa mwanzoni mwa kipindi cha pili.

Klopp amedai jeraha hilo si kubwa lakini bado hana uhakika kuhusu kupatikana kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa katika mechi muhimu dhidi ya Manchester City itakayochezwa kesho.

Kocha huyo wa Ujerumani aliiambia TNT Sports: "Bado hatujui.

"Ibou aliniambia aliponipita wakati huo, 'Nilifikiri ikiwa nitafanya mbio nyingine basi inaweza kuwa mbaya.'

"Anapaswa kuwa sawa kucheza Jumapili lakini hatujui. Joe Gomez yuko sawa, amecheza sana.

"Basi tuone na Ibou. Uingizwaji wake ulikuwa wa tahadhari."

Darwin Nunez alikuwa nyota wa mchezo katika ushindi wa kuvutia wa Liverpool wa Prague, mshambuliaji huyo wa Uruguay akifunga mabao mawili zaidi.

Na la kwanza kati yao, bao la mguu wa kulia kutoka umbali, lilikuwa la mita 1,000 la utawala wa Klopp Liverpool.




## Arteta asisitiza anahitaji straika

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amethibitisha kiwango cha karibuni cha ufungaji wa klabu hiyo haubadilishi mipango ya kusajili mshambuliaji mpya katika dirisha la majira ya joto.

Washikabunduki hao wamekuwa timu ya kwanza katika historia ya miaka 136 ya soka la Ligi Kuu England kufunga mabao matano au zaidi katika mechi tatu mfululizo za ugenini walipoichapa Sheffield United 6-0 Jumatatu iliyopita.

Wakiwa nyumbani wiki za hivi karibuni, pia wamefunga mabao manne dhidi ya Newcastle, matatu dhidi ya Liverpool na manne dhidi ya Crystal Palace.

Lakini nia ya kuzama sokoni kwa mshambuliaji bado iko pale pale.

"Hapana, mipango tuliyonayo kwa majira ya joto iko wazi sana na ilifanyika karibu mwanzoni mwa msimu, kuelewa kile tunaweza kuwa nacho, hali ya mikataba tuliyonayo na baadhi ya wachezaji na jinsi tunavyotaka kuboresha na kudumisha kiwango cha timu," alisema Arteta.



"Kufunga mabao mengi hivi karibuni hakika hakujabadilisha chochote."

Arsenal walitumia pauni milioni 45 kumnunua Gabriel Jesus mwaka 2022 na Mbrazil huyo analeta nguvu zake kwenye timu, lakini kufunga mabao mara kwa mara sio moja wapo.

Wameshiriki mabao mengi badala yake, huku Bukayo Saka, Gabriel Martinelli na Martin Odegaard wote wakifunga mara 15 katika mashindano yote msimu uliopita.

Saka amefikisha magoli 16 tayari mnamo 2023/24, lakini Leandro Trossard (10) ndiye mchezaji mwingine pekee aliyepata takwimu mbili.

Kwa ujumla, wanakosa mwelekeo thabiti katika jukumu la 'namba tisa' kama Manchester City ilivyo na Erling Haaland.

Arsenal kwa muda mrefu imekuwa ikivutiwa na Ivan Toney wa Brentford lakini bei iliyopunguzwa iliondoa uwezekano wa kumsajili Januari.

Bosi wao Thomas Frank amethibitisha mshambuliaji huyo wa England ambaye mkataba wake unamalizika 2025, huenda akauzwa mwishoni mwa msimu huu.

Arteta alikataa kuhusishwa na Toney: "Siongei kuhusu mchezaji mwingine yeyote kwa sababu kama sivyo ni lazima nimtenge kila mchezaji sokoni kwa sababu tunahusishwa na wachezaji wengi."

HABARI MICHEZO

# TANZANITE KAMILI KUWAVAA UGANDA ALL AFRICAN GAMES

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), inarusha karata yake ya kwanza katika mashindano ya All Africa Games kwa kuivaa Uganda leo kwenye Uwanja wa Cape Coast Sports ulioko nchini Ghana.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 2:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Tanzanite imepangwa Kundi A ikiwa pamoja na wenyeji Ghana na Ethiopia ambao walikutana jana jioni.

Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yameenda vizuri na wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya kupambana kuanza vyema mashindano hayo.

Shime alisema mechi hiyo dhidi ya Uganda anatarajia itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao na kufahamiana.

Kocha huyo alisema hana hofu na mechi hiyo kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kikosi chake ambacho kitaingia dimbani kwa ajili ya kusaka ushindi.

"Maandalizi yalifanyika tangu nyumbani, hapa nchini Ghana tumekuja kuweka mipango yetu ya kimbinu na kiufundi kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya Uganda," alisema Shime.

Aliongeza anaimani na vijana wake ambao wana morali nzuri ya kuwakabili wapinzani wao na kila mmoja anahitaji kuweka rekodi ya kushinda mchezo wa kwanza wa mashindano hayo.

Naye nahodha wa Tanzanite, Irene Kisisa, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanaahidi kupambana ili kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Kisisa alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na malengo yao ni kusonga mbele katika mashindano hayo yaliyoanza jana jijini Accra.

„Kila mechi ni muhimu, tunawaheshimu wapinzani wetu, tutacheza nao kwa nidhamu na hatutafikiria matokeo ya nyuma, tunafahamiana kwa sababu tunakutana katika mashindano ya CECAFA," alisema Kisisa.

Baada ya mechi ya leo, Tanzanite itashuka tena uwanjani kuvaana na wenyeji Ghana mechi itakayochezwa Machi 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa Cape Coast na itamaliza hatua hiyo ya awali Machi 15, kwa kupambana na Ethiopia kwenye Uwanja wa Elmina.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya kimataifa ya COSAFA yatakayofanyika baadaye mwezi huu nchini Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

# KMC yasaka rekodi ya 2024

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa KMC umesema wameweka nia ya kuhakikisha wanapata ushindi wa kwanza mwaka huu katika mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa KMC, Khalid Chukuchuku, aliliambia gazeti hili baada ya muda mrefu timu yao kutopata ushindi, sasa wamejipanga vyema kumaliza ukame unaowakabili, na wanawaonya wapinzani wao kujiandaa kukutana na ‚siku ngumu' katika soka.

„Tunakwenda kucheza dhidi ya Tabora United, mechi ya kwanza tulitoa sare, tunajua wana timu nzuri lakini sisi KMC tunazihitaji zaidi pointi tatu kuliko wao na tutakuwa nyumbani.

Tumeshuka hadi nafasi ya sita tukiwa na pointi 25, wenzetu Coastal Union na Prisons wametupita, hapo utaona kabisa tunahitaji ushindi ili tuwafuate juu, kuna nafasi ya nne pale inapiganiwa na inaonekana kutakuwa na vita kubwa sana ili kuipata," alisema Chukuchuku.

KMC itashuka uwanjani kupigania ushindi wa kwanza mwaka huu, mara ya mwisho ilipata ushindi Desemba 2, mwaka jana baada ya kuifunga Mashujaa FC mabao 3-2, na tangu hapo imecheza mechi tisa bila kupata ushindi wowote, ikitoa sare sita na kupoteza michezo mitatu.

Mechi zilizofuata KMC ilichapwa mabao 5-0 dhidi ya Azam, mabao 3-0 na Yanga na Jumanne iliyopita ilipoteza dhidi ya Ihefu kwa kufungwa goli 1-0.

## Mgunda akanusha kutakiwa Singida

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amekanusha taarifa yuko katika mipango ya kujiunga na Singida Fountain Gate inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mgunda ambaye ni Mkurugenzi wa Ufundi wa Simba, alisema hajafanya mazungumzo na kiongozi yoyote wa Singida Fountain Gate na hafahamu chochote kuhusu mchakato huo.

Mgunda alisema hajui taarifa hizo zimetokea wapi na kuongeza yeye bado ni mwajiriwa na Simba.

„Siku zote kocha kutakiwa na timu nyingine ni kawaida, lakini mpaka sasa sijui lolote kuhusu kutakiwa na Singida Fountain Gate kwa sababu hawajaja kwangu, hivyo siwezi kuongea chochote kuhusu hilo," alisema kocha huyo wa zamani wa Coastal Union.

Kocha huyo mkongwe nchini alisema atakuwa katika nafasi ya kuelezea hatima yake pale muda utakapofika na kwa sasa hana lolote la kufafanua.

„Kuhusu kama wakija nitafanya nini, hiyo ni ramli, na kama wakija kuna mengi ya kufanya, ambayo ni mazungumzo, maelewano, kila upande uridhike, kuna matakwa ya kutekelezwa au kutotekelezwa, hapo utaona mlolongo ni mrefu sana, lakini ni mpaka kwanza waje kama ni kweli, kwa sababu narudia tena sijapata taarifa yoyote kuhusu hilo," Mgunda alisema.

Baada ya Singida Fountain Gate kutimua benchi lote la ufundi akiwamo aliyekuwa Kocha Mkuu, Thabo Senong, tetesi zilienea timu hiyo huenda ikamtangaza Mgunda kubeba mikoba ya kuiongoza klabu hiyo.

Timu hiyo kwa sasa ipo chini ya Ngawina Ngawina, akikaimu hadi watakapoikabili Simba Jumanne ijayo, kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Singida FG, Hussein Massanza, watatangaza kocha mpya.

Mara ya mwisho timu hiyo kupata ushindi ilikuwa ni Novemba 27, mwaka jana ilipoifunga Coastal Union mabao 2-1, tangu hapo haijaonja ladha ya ushindi ikicheza mechi nane, ikipoteza tano na kutoa sare tatu.

Desemba Mosi mwaka jana, ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania, na sare nyingine na KMC, kabla ya kwenda kukutana na kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Geita Gold, ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, ikapokea kipigo kingine cha mabao 3-1 kutoka kwa Prisons, na kwenda kutoa sare ya bao 1-1 dhidi ya Taboara United.

Baada ya hapo ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Azam kabla ya kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Michezo
Jumamosi Machi 9, 2024
Nipashe

Haaland aeleza hisia kutwaa mataji matatu UKURASA 21






Kiungo Mkongomani wa Yanga, Maxi Nzengeli (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Namungo FC, Jacob Masawe, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi jana. Yanga ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA KILELENI

## ●●●Ni baada ya kuichapa Namungo, huku Aziz Ki akiendelea kutupia...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Yanga wamerejea tena katika kilele cha msimamo wa ligi hiyo baada ya kutoa kipigo cha mabao 3-1 kwa Namungo, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, Lindi jana.

Ushindi wa Yanga jana umeifanya timu hiyo kufikisha pointi 46, ikiipiku Azam FC yenye pointi 44 ambayo ilikuwa ikiongoza ligi hiyo, ingawa vinara hao wamecheza mechi 17, huku Azam ikiwa imeshashuka dimbani katika michezo 20 mpaka sasa.

Kiungo mshambuliaji wa Yanga raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, alifunga bao moja akifikisha magoli 11, pungufu ya kinara wa sasa, Feisal Salum ‚Fei Toto' wa Azam, Mudathir Yahaya akipachika goli la saba msimu huu huku straika Clement Mzize akifikisha mabao manne.

Beki wa Yanga kutoka Zanzibar, Ibrahim Hamad ‚Bacca' alijifunga mwenyewe na kufanya idadi ya mabao ya kujifunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa kufikia matano.

Mabingwa hao walilazimika kusubiri hadi dakika ya 53 walipohesabu bao la kwanza kupitia Mudathir baada ya kwenda mapumziko wakiwa hawajafungana.

Kiungo huyo ambaye siku za karibuni amekuwa na uwezo wa kufumania nyavu, alipachika bao baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Augustin Okra, aliyeambaa na mpira wingi ya kulia, akauachia mpira kwa Stephane Aziz Ki, ambaye naye hakuwa mchoyo, akampenyezea mfungaji aliyeuweka wavuni kirahisi.

Iliwachukua dakika tatu Yanga kuandika bao la pili, safari hii likiwekwa nyavuni na Mzize, ambaye alimnyang'anya mpira Derrick Mukombozi na kwenda kumsabahi kipa wa Namungo, Jonathan Nahimana, kwa kuukwamisha mpira wavuni.

Safari hii mfungaji ni Aziz Ki, mpira ukianzia kwa Mudathir, akaupeleka kwa Yao Kouassi ambaye aliondoka kwa kasi na kumpa pasi ya upendo mfungaji aliyeumalizia wavuni.

Bacca alijikuta akiusukumiza mwenyewe mpira ndani ya wavu kutokana na krosi ya Emmanuel Charles dakika ya 70 ya mchezo.

Yanga ilifika kwa mara ya kwanza langoni kwa Namungo dakika ya 11, baada ya Okra kuambaa na mpira wenye wingi ya kushoto, kabla kumimina majaro, ambapo shuti la kushoto la muunganishaji, Aziz Ki, lilikosa shabaha na mpira kutoka nje sentimeta chache.

Beki, Mukombozi alifanya kazi ya ziada dakika ya 18, alipouwahi mpira wa krosi ya Yao Kouassi kabla haujamfikia Clement Mzize aliyekuwa anausubiri aukwamishe wavuni, akautoa nje na kuwa kona.

Kipa raia wa Burundi, Nahimana alifanya kazi ya ziada dakika tano kabla ya mapumziko, aliporuka pembeni kama nyani, kulifuata shuti kali la kushtukiza lililopigwa na Salum Aboubakar ‚Sure Boy.'

Kipindi cha pili, Yanga ilionekana kuingia na kuanza kucheza mpira wa kasi zaidi tofauti na kipindi cha kwanza, na iliwalipa kwa kupata mabao hayo.

Dakika 20 kabla mechi kumalizika, Namungo ilionekana kubadilika na kufanya mashambulizi mfululizo, lakini wachezaji wake hawakuwa makini na walikuwa wanapiga mashuti yao nje, licha ya kubaki na kipa, Metacha.

Kwa matokeo hayo, Namungo inabaki nafasi ya saba kwa pointi 23, ikiwa imecheza mechi 20.

## Simba, Coastal kumaliza ubishi

**Na Saada Akida**

IKIWA bila ya Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha aliyerejea kwao Algeria, Simba inatarajia kukutana na Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 12:00 jioni kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani Tanga jijini Tanga.

Benchikha aliondoka nchini Machi 7, mwaka huu na kurejea kwao kwa ajili ya kuhudhuria darasa maalumu la kuongeza taaluma yake ya ukocha ambalo limeandaliwa nchini humo.

Simba itashuka dimbani ikiwa na jeraha la kupoteza mechi yake iliyopita dhidi ya Tanzania Prisons kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1, inahitaji ushindi ili kurejesha furaha kwa mashabiki na wanachama wake.

Simba pia leo itakosa huduma ya beki wao, Henock Inonga, aliyeumia katika mazoezi na kurejeshwa Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu, huku habari njema ikiwa ni kurejea kwa Wilson Onana, ambaye amepona majeraha yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema siku zote Coastal Union wanapokuwa nyumbani kwao mechi inakuwa ngumu na sasa itachagizwa na matokeo yao ya mwisho.

Matola alisema mechi hiyo pia itakuwa na ushindani na kwa kufahamu hilo, Simba imejiandaa kukabiliana na ugumu na ubora wa wapinzani wao ili kupata matokeo chanya.

Naye kipa wa Simba, Ally Salim, alisema wako tayari kukabiliana na Coastal Union na wamejiandaa kupambana ili kuhakikisha wanavuna alama tatu muhimu.

"Baada ya kupoteza mechi ya kwanza presha imekuwa kubwa sana kwa wachezaji lakini tumejiandaa kusahau matokeo ya nyuma, tunahitaji ushindi katika mchezo wa kesho (leo). Hatujakata tamaa bado ligi ni ndefu na kikubwa tunahitaji kushinda mechi zilizopo mbele yetu," alisema kipa huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, David Ouma, alisema baada ya kuvuna pointi moja ugenini wamerejea nyumbani kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya dhidi ya Wekundu wa Msimbazi.

"Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu wapinzani wetu Simba wametoka kupoteza mechi hivyo wanahitaji matokeo, lakini hata sisi pia tunahitaji kutafuta alama muhimu na kuhakikisha tunatumia vizuri uwanja wa nyumbani," alisema Ouma.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >